# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

## ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR 2020 - 2025

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Zubeir Ali Maulid | - | SPIKA |
| 2. | Mhe. Mgeni Hassan Juma | - | Naibu Spika/Nafasi za Wanawake |
| 3. | Mhe. Mwanaasha Khamis Juma | - | Jimbo la Dimani |
| 4. | Mhe. Shaaban Ali Othman | - | Jimbo la Mpendae |
| 5. | Mhe. Hemed Suleiman Abdulla | - | MBM/Makamu wa Pili wa Rais/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Uteuzi wa Rais |
| 6. | Mhe. Mudrik Ramadhan Suleiman (OR) | - | MBM/Waziri wa Nchi, Kazi, Uchumi na Uwekezaji/ Jimbo la Bububu. |
| 7. | Mhe. Masoud Ali Mohammed (OR) | - | MBM/Waziri wa Nchi, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Ole. |
| 8. | Mhe. Haroun Ali Suleiman (OR) | - | MBM/Waziri wa Nchi, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora/Jimbo la Makunduchi. |
| 9. | Mhe. Jamal Kassim Ali (OR) | - | MBM/Waziri wa Nchi, |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | Fedha na Mipango/Jimbo la Magomeni. |
| 10. Mhe. | Dkt Khalid Salum Mohamed | - | MBM/Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi/Jimbo la Donge. |
| 11. Mhe. | Dkt. Soud Nahoda Hassan | - | MBM/Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo/Jimbo la Paje |
| 12. Mhe. | Simai Mohammed Said | - | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Tunguu |
| 13. Mhe. | Tabia Maulid Mwita | - | MBM/Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo/ Uteuzi wa Rais |
| 14. Mhe. | Riziki Pembe Juma | - | MBM/Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi/ Nafasi za Wanawake |
| 15. Mhe. | Rahma Kassim Ali | - | MBM/Waziri Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi/Nafasi za Wanawake |
| 16. Mhe. | Suleiman Masoud Makame | - | MBM/Waziri wa Maji, Nishati na Madini/Jimbo la Chonga |
| 17. Mhe. | Abdulla Hussein Kombo | - | MBM/Waziri wa Uchumi wa Bluuu na Uvuvi /Jimbo la Mkoani |
| 18. Mhe. | Lela Muhamed Mussa | - | MBM/Waziri wa Utalii na |

Mambo ya Kale/Nafasi za Wanawake

19. Mhe. Abdalla Abasi Wadi - Jimbo la Nungwi
20. Mhe. Ali Abdulgulam Hussein - Jimbo la Jang'ombe
21. Mhe. Ali Suleiman Ameir - Jimbo la Pangawe
22. Mhe. Ameir Abdalla Ameir - Jimbo la Mwanakwerekwe
23. Mhe. Anna Athanas Paul - Uteuzi wa Rais
24. Mhe. Asha Abdalla Mussa - Jimbo la Mahonda
25. Mhe. Azza Januar Joseph - Nafasi za Wanawake
26. Mhe. Bahati Khamis Kombo - Jimbo la Chambani
27. Mhe. Bakar Hamad Bakar - Jimbo la Wawi
28. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Nafas iza Wanawake
29. Mhe. Fatma Ramadhan Mohamed (Mandoba) Nafasi za Wanawake
30. Mhe. Habibu Ali Muhamed - Jimbo la Mtambwe
31. Mhe. Haji Omar Kheri - Jimbo la Tumbatu
32. Mhe. Haji Shaaban Waziri - Jimbo la Uzini
33. Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Kwamtipura
34. Mhe. Harusi Said Suleiman - Jimbo la Wete
35. Mhe. Hassan Hamad Omar - Jimbo la Kojani
36. Mhe. Hassan Khamis Hafidh - Jimbo la Welezo
37. Mhe. Hudhaima Mbarak Tahir - Nafasi za Wanawake
38. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu - Jimbo la Mtoni
39. Mhe. Juma Makungu Juma - Jimbo la Kijini
40. Mhe. Juma Ali Khatib - Uteuzi wa Rais
41. Mhe. Issa Haji Ussi Gavu - Jimbo la Chwaka
42. Mhe. Kombo Mwinyi Shehe - Jimbo la Wingwi
43. Mhe. Machano Othman Said - Jimbo la Mfenesini
44. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando
45. Mhe. Mihayo Juma Suleiman - Jimbo la Mwera
46. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni
47. Mhe. Mohamed Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile
48. Mhe. Mohamed Ahmada Salum - Jimbo la Malindi
49. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
50. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
51. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
52. Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis - Nafasi za Wanawake

| | | | |
|---|---|---|---|
| 53. Mhe. | Mwanajuma Kassim Makame | - | Nafasi za Wanawake |
| 54. Mhe. | Dkt. Mwinyi Talib Haji | - | Mwanasheria Mkuu |
| 55. Mhe. | Nadir Abdullatif Yussuf | - | Jimbo la Chaani |
| 56. Mhe. | Nassor Salim Ali | - | Jimbo la Kikwajuni |
| 57. Mhe. | Nassor Ahmed Mazrui | - | Uteuzi wa Rais |
| 58. Mhe. | Omar Said Shaaban | - | Uteuzi wa Rais |
| 59. Mhe. | Panya Ali Abdalla | - | Nafasi za Wanawake |
| 60. Mhe. | Rukia Omar Ramadhan | - | Jimbo la Amani |
| 61. Mhe. | Saada Ramadhan Mwendwa | - | Nafasi za Wanawake |
| 62. Mhe. | Dkt. Saada Mkuya Salum | - | Uteuzi wa Rais |
| 63. Mhe. | Saidi Saleh Salim | - | Jimbo la Tumbe |
| 64. 5Mhe. | Sabiha Filfil Thani | - | Nafasi za Wanawake |
| 65. Mhe. | Salha Mohamed Mwinjuma | - | Nafasi za Wanawake |
| 66. Mhe. | Salma Mussa Bilal | - | Nafasi za Wanawake |
| 67. Mhe. | Suleiman Makame Ali | - | Jimbo la Ziwani |
| 68. Mhe. | Suleiman Haroub Suleiman Samaki | - | Jimbo la Kiembe |
| 69. Mhe. | Sulubu Kidongo Amour | - | Jimbo la Mkwajuni |
| 70. Mhe. | Shadya Mohamed Suleiman | - | Nafasi za Wanawake |
| 71. Mhe. | Shamata Shaame Khamis | - | Jimbo la Micheweni |
| 72. Mhe. | Shaib Hassan Kaduara | - | Jimbo la Chake Chake |
| 73. Mhe. | Yahya Rashid Abdulla | - | Jimbo la Kwahani |
| 74. Mhe. | Yussuf Hassan Iddi | - | Jimbo la Fuoni |
| 75. Mhe. | Zaina Abdalla Salum | - | Nafasi za Wanawake |
| 76. Mhe. | Zawadi Amour Nassor | - | Jimbo la Konde |

**Ndg. Raya Issa Msellem - Katibu**

**Kikao cha Saba - Tarehe 22 Februari, 2021**

*(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)*

**DUA**

*Mhe. Naibu Spika (Mgeni Hassan Juma) alisoma dua*

## TAARIFA YA SPIKA

Waheshimiwa Wajumbe katika kikao cha Baraza cha tarehe 15 Februari, 2021 Mhe. Miraji Khamis Mussa aliuliza swali la nyongeza lililotokana na swali la msingi Nam. 19 na Mhe. Waziri wa Maji, Nishati na Madini aliahidi kujibu swali hilo kwa maandishi. Sasa namuomba Mhe. Waziri wa Maji, Nishati na Madini asome jibu la swali la nyongeza lililoulizwa na Mjumbe huyo.

**Mhe. Waziri wa Maji, Nishati na Madini:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, awali ya yote naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuamka salama.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kujibu swali la nyongeza lililoulizwa na Mhe. Miraji Khamis Mussa aliyetaka kujua gharama za kusambaza umeme katika kijiji cha Chanjaani.

Mhe. Naibu Spika, gharama za kusambaza umeme kwenye kijiji cha Chanjaani ni fedha za Kitanzania shilingi milioni 75 zinazojumuisha na *transformer* pamoja na *low voltage.* Mheshimiwa naomba kuwasilisha.

## TAARIFA YA SERIKALI

### Hotuba ya Mwelekeo wa Hali ya Uchumi, Mpango wa Maendeleo na Bajeti kwa Mwaka 2021/2022 - 2023/2024 - Wizara ya Nchi (OR) Fedha na Mipango

*(Majadiliano yanaendelea)*

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yanaendelea tulikuwa tuna Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis anachangia, lakini kwa mujibu wa muda ambao tulionao Mhe. Mwantatu alikuwa hajamaliza kuchangia. Kwa hivyo, kwanza nimpe Mhe. Mwantatu, baada ya hapo ajitayarishe Mhe. Haji Omar Kheri na atafuata Mhe. Rukia Omar Ramadhan. Mhe. Mwantatu karibu.

**Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia hotuba ya Mwelekeo wa Hali ya Uchumi, Mpango wa Maendeleo na Bajeti kwa mwaka 2021/2022 - 2023/2024.

Mhe. Spika, awali ya yote kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuamka tukiwa na hali ya usalama ndio tukaendelea na utaratibu kama tuliojipangia. Lakini kwa kuendelea na mchango wangu Mhe. Naibu Spika, nilikuwa nazungumzia suala zima la kuimarisha uchumi nilianzia kuchangia kuhusiana na kikosi chetu cha JKU lakini sasa naendelea na Chuo chetu cha Mafunzo. Ningeomba Serikali kupitia Chuo cha Mafunzo kujiimarisha zaidi katika kilimo ili kuzalisha chakula cha kuweza kuwahudumia wanafunzi,

lakini pia waweze kuzalisha kilimo kwa ajili ya biashara na waweze kufikia malengo yao mengine, lakini pia itapunguza utegemezi kwa Serikali kuu. Lakini pamoja na hayo, waweze kuimarisha viwanda ambavyo wanavyo, wana viwanda vya uchongaji pamoja na ushoni ili kujiimarisha zaidi vikosi vyetu hivi viweze kuangalia maeneo hayo.

Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 15 ukurasa wa 23 kipaumbele namba saba kinaelezea kuendelea na utekelezaji wa programu ya ajira kwa vijan. Nichukue nafasi hii kuipongeza sana serikali kwa kuona umuhimu wa kuendeleza programu hii na kuwa moja ya kipaumbele chake. Programu hii ina umuhimu mkubwa kwa vijana na imejenga matumaini makubwa sana kwa vijana, lakini ndio programu ambayo kipindi kilichopita ilikumbwa na mtihani mkubwa sana, tukiangalia mradi wa pili pili ambao ulitumia gharama kubwa lakini haukuwa na mafanikio yoyote. Lakini pia katika programu hii kulikuwa na programu ya kujenga *green house* katika kila wilaya. Cha kusikitisha Mheshimiwa fedha nyingi imetumika katika kutengeneza *green house* lakini hakuna hata moja mpaka sasa hivi ambayo imeleta tija. Vile vile katika kuendeleza programu hii kumetolewa fedha kwa ajili ya kununulia vifaa kuna mjumbe alisema hapa hata hivyo vifaa vilivyotolewa vyengine ni vibovu.

Lakini isitoshe katika kuendeleza programu hii walitakiwa vijana kutoa au kueleza mahitaji yao, kilichofanyika ni tofauti vijana wamepelekewa vifaa ambavyo sivyo walivyovihitaji, kwa maana hiyo sifikirii kama katika programu zote hizo na shughuli zote hizo zimeleta tija. Kwa hivyo, naomba niishauri Serikali yangu kupitia Mhe. Waziri kutoa wataalam wake kwa huko tunakokwendea fedha ambazo zitaingizwa kwa programu ya ajira kwa vijana na miradi ambayo itaibuliwa lazima ifanyiwe utafiti wa kina, ili ijulikane uwezo wake na vipi itaendelea. Si vibaya kama tutaona miradi haiwezi kuendelea basi tukawashauri vijana vizuri kwa sababu lengo la serikali ni kuwaendeleza, sio kutoa pesa na kutumika ikawa imekwisha, zinatolewa fedha nyingi za serikali kwa ajili ya kuendeleza vijana na kuzalisha ajira kwa vijana.

Kwa hivyo, endapo pesa zitakuwa zinatolewa halafu zinatumika na maendeleo hakuna na kile kilichotumika haionekani faida yake, sifikirii kama malengo yanaweza kufikiwa. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kulifanyia kazi suala hili hasa katika kufanya utafiti wa miradi ya vijana ambayo itaibuliwa.

Mhe. Naibu Spika, niendelee kwa kuzungumzia suala zima la maendeleo, hatuwezi kuzungumzia maendeleo tukaacha makundi mengine, kuna miradi mingi ya maendeleo humu kuna majengo ya maskuli, kuna miradi mingi tu ambayo lengo ni kunufaisha wananchi wote. Niiombe serikali tunapojenga majengo ya umma tuzingatie mahitaji ya watu wenye ulemavu. Kuna majengo mengi ya umma yamejengwa hayafikiki na watu wenye ulemavu, mfano Wizara ya Wanawake na Watoto imejengwa juzi tu, lakini unapowaambia watendaji wanasema tulisahau na hii yote inakuja kutokana na kwamba sheria namba 9 ya mwaka 2006 ya watu wenye ulemavu haifanyiwi kazi. Pamoja na kuwa haifanyiwi kazi Mhe. Naibu Spika, sheria hii ina mapungufu makubwa na tumeshasema sana humu Barazani kwamba sheria ile iletwe ifanyiwe marekebisho iendane na wakati, ili haki za watu wenye ulemavu ziweze kupatikana kama ilivyo katika sheria. Mapungufu ya sheria ile yanapelekea haki za watu wenye ulemavu nyingi kukosekana. Kwa hivyo, niiombe serikali miongoni mwa sheria ambazo zinatakiwa kufanyiwa marekebisho basi na sheria namba 9 ya mwaka 2006 iwe ni kipaumbele mwa sheria ambazo zitafanyiwa marekebisho.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea nakuja katika suala zima la ukusanyaji wa mapato, serikali imejipanga katika kusimamia upatikanaji wa mapato, lakini naishauri serikali bado itilie

mkazo kusimamia kwanza vituo vyetu vya kuuzia mafuta hawaoni umuhimu wao wa kutoa risiti na hazitolewi risiti mpaka uombe. Mimi nafikiri suala hili ni zito linahitaji usimamizi. Niombe wale wote waliopewa jukumu na dhamana ya kusimamia hili walisimamie vizuri, bado vituo vyetu vya kutoa mafuta havitoi risiti mpaka uombe na wao wajibu wao mtu anapotumia wampe risiti na wananchi sio wote ambao watakuwa na mwamko wa kusema nipe risiti kwa hivyo mapato yanapotea. Halikadhalika na wauza maduka sio wote ambao wanatoa risiti hadi sasa kwa hivyo naomba na hili pia lisimamiwe.

Mhe. Naibu Spika, mpango ni mzuri, mpango una malengo makubwa kwa maslahi ya wananchi naunga mkono kwa asilimia mia moja. Naunga mkono viongozi wetu akiwemo Rais wetu Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi Mwenyezi Mungu ampe nguvu zaidi, ili malengo yote haya yaliyopangwa humu yaweze kutekelezeka na maslahi kwa wananchi wetu yaimarike. Ahsante sana nakushukuru Mhe. Naibu Spika.

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante Mheshimiwa naomba sasa nimwite Mhe. Rukia Omar Ramadhan baadae ajitayarishe Mhe. Yahya Rashid Abdalla.

**Mhe. Rukia Omar Ramadhan:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hotuba ya Mwelekeo wa Hali ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo na Bajeti kwa mwaka 2021/2022 - 2023/2024. Awali ya yote na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia afya njema na kuweza kuja kutimiza wajibu wetu wa kikatiba.

Pili, nitoe pole kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi kwa msiba mkubwa uliotukuta kuondokewa na Makamu wa Kwanza wa Rais. Niwape pole pia chama cha *ACT* Wazalendo, familia, ndugu, jamaa na Wazanzibari wote. Mwenyezi Mungu amlaze mahala pema na sisi atujaalie hatima njema.
Amin.

Mhe. Mwenyekiti, nianze pia kumpongeza Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha na Mipango pamoja na watendaji wa wizara hii kwa kutimiza wajibu wao wa matakwa ya kikatiba kutuletea huu mpango kwa wakati nawapongeza sana kwa hilo.

Mhe. Naibu Spika, nianze mchango wangu mimi katika hotuba hii nimeona imo katika makundi matatu. Kwanza, ukuaji wa uchumi, ukusanyaji wa mapato, upunguzaji wa umaskini, upunguzaji wa matumizi yasiyo ya lazima ya serikali. Pili, huduma na ustawi wa jamii, afya, elimu, maji, miundombinu na ushirikishwaji wa jamii. Tatu, utawala bora na umoja wa kitaifa. Napongeza sana kwani imekidhi mahitaji yote tunawaombea Mwenyezi Mungu mpango huu uje utekelezeke ili tupate manufaa mazima kwa taifa letu.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuchangia kwenye ukurasa wa 3 kifungu kidogo cha 4 kwenye kipengele kinachozungumza hatua nyengine zilizotumika katika kuimarisha mapato ya serikali na kusaidia kurahisisha shughuli za kibiashara. Mchango wangu upo kwenye tozo na ada zote kwa wafanyabiashara wadogo wadogo. Katika kitabu hichi imezungumzwa kwamba wafanyabiashara hawa wanatakiwa walipe shilingi elfu thalathini kwa mwaka (30) badala ya shilingi elfu moja hadi elfu mbili kwa siku. Lakini wafanyabiashara hawa hivi sasa wanalipa zaidi ya shilingi elfu thalathini, wanatozwa shilingi elfu moja kwa siku ukijumlisha kwa mwaka ni shilingi laki tatu sitini (360,000/=) na baadhi ya wengine wanalipa kodi ya kibaraza shilingi elfu thalathini mpaka elfu sitini. Je, serikali ina mpango gani wa kutekeleza suala hili la kupunguza tozo kama ilivyoelezwa kwenye kitabu hichi hasa ukizingatia wafanyabiashara hawa ni wadogo.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye ukurasa wa tatu kifungu kidogo cha 5 kwenye kipengele kinachozungumzia hatua nyengine zilizotumika katika kuimarisha mapato ya serikali na kusaidia kurahisisha shughuli za kibiashara. Kwa mujibu wa maelezo, hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kupunguza kiwango cha ada ya usajili wa uwekezaji kinachotozwa na *ZIPA* kutoka dola 500 hadi dola 200, kiwango kinachotozwa hadi sasa ni dola 500. Je, serikali ina mpango gani wa kupunguza kodi hiyo kama walivyoeleza kwenye kitabu hicho.

Mhe. Naibu Spika, mchango wangu unaelekea ukurasa wa 19 katika kipengele cha matarajio ya ukuaji, nashauri tuongeze kipengele kimoja ukusanyaji wa mapato utumike kwa kutumia mfumo wa electroniki ili kuweza kudhibiti upotevu na kukuza mapato.

Mhe. Naibu Spika, niko hapo hapo katika ukurasa wa 19 kipengele cha shabaha na malengo ya uchumi kwa mwaka 2021-2023. Katika kipengele cha msingi, nashauri tuongeze kipengele kinachoonesha wananchi nao wanawajibika katika kuongeza uchumi, maana vipengele vilivyopo vinawalenga wafanyakazi pekee bila ya wananchi nao kuwajibika, kwani suala hili la uchumi itakuwa ni ndogo bila ya kuwashirikisha wananchi.

Mhe. Naibu Spika sasa naomba kuchangia ukurasa wa 23 kipengele cha 6 kuimarisha sekta mtambuka. Nashauri kuongezwe kipengele cha kukabiliana na maafa kwani sote tunaelewa kwamba maafa ni suala lisilotabirika.

Mhe. Naibu Spika, niende ukurasa wa 25 kipengele cha 17 mwelekeo wa matumizi. Katika mwelekeo huu wa matumizi inaonesha kuwa hatutokuwa na akiba ya mapato, maana katika hotuba inaonesha tunachokikusanya ndicho tutakachokitumia. Je, serikali haioni hiyo ni hatari kutokuwa na akiba.

Mhe. Naibu Spika, niishauri serikali katika sehemu ambazo tunaweza kuokoa fedha tukiweza kudhibiti au kuweka mpango mzuri katika matumizi sahihi ni lazima tuzibe mianya ya matumizi na uvujaji wa mapato yasiyo ya lazima. Ushauri wangu uko hapa, tuangalie utaratibu mzuri wa safari za nje za viongozi wakuu pamoja na watendaji, tuwe na utaratibu mzuri wa ununuzi wa *stationery*. Hapo awali ilikuwa inafanywa na Wakala wa Serikali kwa kupitia mpango wa manunuzi. Tuangalie pia kwenye sehemu ya matengenezo ya magari ya serikali, nashauri pia iwezeshwe ijengewe uwezo Karakana ya Serikali, ili magari yote ya serikali yawe yanatengenezwa katika karakana hiyo. Twende pia kwenye matumizi ya mafuta ya serikali, nashauri kiwepo kituo maalum katika wilaya ama mikoa ili mafuta hayo yawe yanakwenda kutiwa katika vituo hivyo.

Pia nashauri katika ujenzi wa majengo ama nyumba za serikali tutumie *resources* ambazo zipo vikosi vyetu vya SMZ tenda hizo tuwape wao tuwajengee uwezo, tuimarishe ili washughulikie hili suala kuliko kuchukua kampuni za nje. Tukitizama wakija hapa wao wanasimamia tu, lakini sisi wenyewe ndio tunaojenga na wao ndio wanaofaidika na fedha ya serikali inapotea. Hii itapunguza matumizi yasiyo sahihi na kupelekea mpango mzuri wa matumizi ambayo utasaidia kuboresha huduma za kijamii pamoja na vipaumbele ambavyo vipo tutaweza kuvitekeleza kwa wakati.

Mhe. Naibu Spika, ili serikali iendelee ni lazima ikusanye kodi na kila mwananchi anatakiwa alipe kodi, hivyo katika suala la ukusanyaji kodi wananchi wangu wa Jimbo la Amani wamenituma hawapingi la serikali kwenye suala hili wapo bega kwa bega na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Ombi lao inapokuja kodi washirikishwe waelimishwe kutokana na kodi ambayo wanatozwa. Hivi karibuni kumetokea wameambiwa

kila kaya ilipe shilingi 3,000 ya usafi hawajapatiwa elimu na wala hawana taarifa ya fedha hizo na kodi hiyo, kwa hiyo wanaomba wao washirikishwe.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie pia kuhusiana na *process* za uhaulishaji ambapo wananchi wengi huwa wanachelewa kufanya uhaulishaji kutokana na muda mrefu ambao wanachukua katika kushughulikiwa suala hili pamoja na *cost* kuwa kubwa. Tunaomba hili nalo lifanyiwe kazi ili huu urasimu upungue wananchi nao waweze kuipata huduma kwa haraka wapende kwenda kufanya uhaulishaji, hii itaboresha mapato yetu ya serikali.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi tunamuombea kheri, baraka na maisha marefu Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, ili aweze kutuongoza vyema kama dhamira yake anayokusudia. Ahsante nashukuru sana. *(Makofi)*

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante mheshimiwa, mchangiaji anayefuata nishamtaja Mhe. Yahya Rashid Abdulla (Mamba) na baada ya hapo ajitayarishe Mhe. Sulubu Kidongo Amour.

**Mhe. Yahya Rashid Abdulla:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia kukutana muda huu tukiwa wazima na afya njema katika Baraza letu hili kwa ajili ya kuchangia Hotuba ya Mwelekeo wa Hali ya Uchumi, Mpango wa Maendeleo na Bajeti kwa mwaka 2021/2022, 2022/2023 na 2023/2024.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu na nitoe pole sana kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kutokana na msiba wa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar. Pia pole zangu hizi zielekee kwa chama chake cha *ACT* Wazalendo, familia yake pamoja na Wazanzibari wote. Mwenyezi Mungu amlaze mahala pema peponi, awarehemu wazazi wetu, lakini nasi atujaalie hatima njema. *(Makofi)*

Mhe, Naibu Spika, hoja yangu katika kitabu hichi kwanza kabla ya kuanza hoja niwashukuru Mhe. Waziri kwa uwasilishaji mzuri lakini pia Mwenyekiti wa Bajeti alipotuwasilishia taarifa hii, wote wawili hao niwapongeze lakini pia niwapongeze wale wote walionitangulia katika kuchangia hotuba hii.

Mhe. Naibu Spika, mchango wangu ninaanzia ukurusa wa 31 ambapo kuna Mpango wa Utekelezaji wa Maendeleo kwa kipindi cha Julai hadi Disemba, 2020 kifungu namba 7 kinaelezea kuendeleza ujenzi wa Mji wa Kisasa wa Kwahani.

Mhe. Naibu Spika, ningelimuomba Mhe. Waziri baadae aje atuelezee kwa sababu kifungu hichi kinaelezea ujenzi hatua iliyofikiwa, lakini wananchi wa Jimbo la Kwahani wakati wa kipindi cha mwezi wa Oktoba kulifanyika makabidhiano ya nyumba zile na walikabidhiwa katika serikali ya Awamu ya Saba na Mhe. Rais wa Zanzibar kwa wakati ule Dkt. Ali Mohamed Shein na katika mwezi ule pia ikatoka ahadi ya serikali. Lakini hadi leo pamoja na maelezo haya wananchi wa Jimbo la Kwahani hawajui hatima yao ni lini nyumba zile watakabidhiwa.

Lakini pia kwa mujibu wa mkataba wa zile nyumba nafikiria mikataba yao imemalizika mwezi wa Januari na sasa hivi tuko Februari. Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri aje atupe maelezo itoke kauli ya serikali wananchi hawa ni kipindi gani watakabidhiwa nyumba zao.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo nakuja katika vipaumbele 2021/2022 - 2023/2024 kuimarisha huduma za kijamii, kifungu (c) kinaelezea kuendeleza ujenzi wa mji wa kisasa kitabu hichi ambacho cha muelekeo. Nashukuru kimetuelezea malengo ya dira hii yanafikiwa na serikali imeanza kutafsiri malengo haya inaendelea na uandaaji wa mpango wa maendeleo kwa muda wa miaka 2021 - 2025. Lakini pia dira ya maendeleo ya 2020 - 2050 na Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya 2020 - 2025 pamoja na hotuba ya Mhe. Rais alipofungua Baraza la Kumi na Wawakilishi.

Hoja yangu ipo hapa, huu ujenzi maeneo yapo mengi ambayo yanatakiwa kujengwa miji ya kisasa na kwa maelezo ya hapa hayajitoshelezi. Nilikuwa namuomba Mhe. Waziri atakapokuja atufafanulie maeneo gani yatakayoweza kupewa kipaumbele, ukizingatia moja ya malengo makuu ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuwapatia huduma bora wananchi. Lakini pia nirudie tena katika mwezi wa Oktoba wakati tumo katika kampeni Chama cha Mapinduzi na serikali yake iliahidi kuendeleza mji ule wa Kwahani.

Kwa hivyo, katika ufafanuzi huu mimi ombi langu sana naomba kipaumbele bado tuendelee katika ujenzi wa mji huu wa Kwahani. Mhe. Waziri atakapokuja hapa atupe ufafanuzi ni maeneo gani ambayo yatapewa kipaumbele cha mwanzo katika ujenzi huo. Lakini Ilani ya Chama cha Mapinduzi na serikali iliahidi kwa wananchi wa Kwahani suala hilo.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo nakuja kipaumbele namba 7(a)(i) kinaelezea juu ya uendelezaji wa masoko sita. Masoko ya Mwanakwerekwe, Chuini, Mombasa, Machomane, Mkokotoni na Jumbi.

Mhe. Naibu Spika, eneo hili pia nitamuomba Mhe. Waziri aje atupe ufafanuzi kwa sababu ukiangalia haya kwa lugha iliyotumika hapa maeneo haya tayari yameshajengwa. Naomba tupate ufafanuzi ni ujenzi gani utakaoendelea hapa. Halikadhalika, namba 7(a)(ii) inaelezea ujenzi wa vituo vya daladala Kijangwani, Chuini na Chanjaani. Uelewa wangu mimi tayari baadhi ya vituo hivi kama Kijangwani, Chuini tayari kuna vituo vya daladala ingawa havikidhi hali tuliyonayo sasa hivi.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri pia tutahitaji maeneo haya lugha iliyotumika hapa maana yake ingelitumika lugha ya kuendeleza ningekuwa sina mashaka, lakini imetumika ujenzi. Kwa hivyo, aje atupe ufafanuzi wa hii yaani nambari 7(a)(i) na (ii).

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo nakuja ukurasa wa 22 vipaumbele kifungu namba 5 Kuimarisha Utawala Bora. Kifungu namba 5 (e) Kuendelea na Juhudi za Uhifadhi wa Mji Mkongwe na Mambo ya Kale, hapa nishauri tu kwa sababu nahisi hii ingelistahiki zaidi kuhamishiwa hapa na kupelekwa katika kuimarisha Sekta Kuu za Uchumi na kuwekwa katika Kuimarisha Utalii kwa wote. Sasa nilikuwa nashauri hii ingelihamishiwa eneo hili na kupelekwa katika kuimarisha Sekta Kuu za Uchumi, Utalii kwa wote. Mhe. Naibu Spika, hasa kipande hichi hapa nilikuwa namuomba Mhe. Waziri waiangalie vizuri nahisi imekaa pahala ambapo sio pake.

Mhe. Naibu Spika, nakuja kipaumbele namba 21 pia na tuanze Kuimarisha Sekta Kuu za Uchumi. Mhe. Naibu Spika, eneo hili pia nitamuomba Mhe. Waziri ufafanuzi kwa sababu hapa kasema kwa wote na ukizungumza utalii kwa wote maana yake unagusa sekta nyingi. Kwa hivyo, pia nataka ufafanuzi zaidi atupe maelezo ni maeneo gani hasa ambayo yatakayozingatiwa na serikali.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie kwa kuimarisha miundo mbinu a, b, c, d, e, f na g hapa nitoe pongezi tu kwa serikali kuonesha utayari wake katika maandalizi ya kuimarisha miundo mbinu na muelekeo wa serikali katika kuinua uchumi kwa nchi yetu. Hapa nitoe pongezi kwa sababu kwa kauli ya Mhe. Rais safari ndio imeanza, lakini baada ya pongezi hizo pana fursa hapa Mhe. Waziri ambazo zitakuwepo.

Mhe. Naibu Spika, niombe fursa hizi ndani ya ilani yetu tumeahidi ajira laki tatu kwa vijana wetu. Tutakapofika kipindi ambacho cha kutumika fursa hizi nafikiri serikali yetu imefika wakati kuwaandaa vijana wetu na tuwe tayari kuweza kuzitumia fursa hizi na kuweza kupunguza tatizo la ajira.

Mhe. Naibu Spika, mwisho nikushukuru na nishukuru uwasilishaji wa taarifa hii ya mpango huu ni mzuri na umeangalia maslahi ya taifa. Naunga mkono kwa asilimia mia moja, ahsante sana. *(Makof)*

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante mheshimiwa, mchangiaji anayefuata ni Mhe. Sulubu Kidongo Amour na ajitayarishe Mhe. Zawadi Amour Nassor.

**Mhe. Sulubu Kidongo Amour:** Mhe. Naibu Spika, kwanza na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu muumba wa mbingu na ardhi, lakini pia namshukuru Mhe. Rais kwa kuchagua mawaziri wazuri wenye afya, wenye akili nzuri, lakini pia namshukuru Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha na Mipango kijana mwenzetu ambaye aliyeleta hoja hii.

Mhe. Naibu Spika, hoja hii mimi naipongeza sana isipokuwa kuna mambo madogo madogo nataka kuchangia kwa ajili ya wananchi na hasa wananchi wa Jimbo la Mkwajuni. Lakini pia natoa pole Makamu wa Kwanza wa Rais katutoka katika muelekeo wa ghafla.

Mhe. Naibu Spika, mimi naelekea kwenye ukurasa wa 20 unaosema Mageuzi ya Uchumi, Maendeleo ya Rasilimali Watu na Huduma za Kijamii. Kuimarisha Miundombinu ya Utawala Bora na Uhimili. Kwa kweli eneo hili kwa serikali yetu ni eneo mama kwa sasa hivi, huko tunakotoka eneo hili liliachwa. Kuna vitu vingi sana hatukuvisimamia kipindi hicho na ndio maana tumeshuka kiuchumi katika mwelekeo. Sasa hivi mawaziri hapa ndio mahala pake pa kusimamia kwa sababu Mhe. Rais amekuja na Uchumi wa Buluu kama hatukusimamia tutakwenda siko.

Mhe. Naibu Spika, natolea mfano Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa Jimbo langu la Mkwajuni kulikuwa na kilimo cha tangawizi na manjano, hichi kilimo sasa hivi hakipo kimeondoka kabisa, kuondoka kwa kilimo hichi kumeleta kutokupatikana hata kile chakula kwa sababu ilikuwa wanawake pale ndio wanaolima kilimo hichi. Kwa kuwa serikali ilisahau kukisimamia kilimo hichi hivi sasa kimeshapotea. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri hapa atumie nguvu zake kwa Wizara ya Kilimo ili hichi kilimo kirudi.

Lakini pia Mhe. Naibu Spika, naelekea kwenye utalii Zanzibar ni watu wa kwanza naweza kusema Afrika tulioanzisha utalii kwa sababu Kenya wao ulikuwepo ukapotea, sisi tukaleta hapa tukaendeleza utalii. Utalii hatukuusimamia vizuri na hatukuusimamia vizuri utalii serikali imepoteza pesa nyingi sana, lakini kwa wananchi kumepotea mambo mengi sana kwa sababu kipindi hicho hicho ulikuja ukulima wa mwani. Mhe. Naibu Spika, ukulima wa mwani ndani ya jimbo langu, ndani ya Jimbo la Kijini, ndani ya Jimbo la Chaani umepotea hakuna tena mwani. Sasa hivi kile chakula cha mwananchi kinampiga chenga kwa sababu mwananchi alikuwa anategemea mwani na kilimo cha manjano na tangawizi, sasa hivi

hamna. Kwa hiyo, iko haja Mhe. Waziri asimamie wizara hizi ambazo zinashughulika na mambo haya ili twende vizuri.

Mhe. Naibu Spika, jengine nakwenda kwenye uvuvi, mheshimiwa ndani ya jimbo langu kwa sababu jimbo langu mimi limepakana na jimbo la Kijini sisi tuna kisiwa na Mnemba, kisiwa hiki kina mambo mawili au matatu. Kisiwa cha Mnemba kina utalii ndani, kisiwa cha Mnemba kimezungukwa na mwamba ambao wananchi wanakwenda kuvua sehemu hizo. Sasa hivi huu utalii, mtalii anapokwenda kule kukoga anakuwa anajipaka madawa katika mwili wake, akizamia yale madawa yanaenea kwenye bahari na yale matumbawe yanaangamia na yale mayai ya samaki yanakwenda.

Kwa hiyo, sasa hivi uvuvi umeshuka samaki ndani ya hiki kisiwa sasa hivi wameshuka, kinachotakiwa hapa kwanza mheshimiwa atengeneze kitu ili wataalamu waende pale kwenda kuangalia yale matumbawe vile ambavyo yanaharibika. Hata hii sehemu ya mwani umepotea kwa sababu ya huu utalii, nakumbuka kipindi kile nilizungumza kuwa kuna madawa ambayo wazungu wanakoga kwenye *swimming pool* sehemu ile ya ufukwe wanamwaga yale maji bahari imeshaharibika kwa hiyo mwani umeumia wote na wale samaki wadogo wadogo kwa maeneo yale hakuna tena. Sasa haya ni mambo ambayo yanatakiwa Mhe. Waziri baadae asimamie haya kwa sababu kitabu alichokitengeneza hiki ametengeneza kitabu kizuri, na hizi pesa za serikali ni nyingi sana zinatumika, lakini kama hazikusimamiwa vizuri basi hatutokuwa na jambo ambalo litalokuwa endelevu.

Mhe. Naibu Spika, naende kwenye suala la elimu, huku tuna Chuo cha Utalii lakini chuo hiki sasa hivi katika utaratibu wetu inawezekana wageni ndio wanakuja kusoma zaidi kuliko wa Zanzibar. Kwa hiyo, hapa panatakiwa kusimamiwa ili twende vizuri katika mwelekeo wa kitabu hiki, Mhe. Waziri hiki kitabu amekitengeneza vizuri sana kila kitu kipo hapa. Lakini usimamiaji ndio muhimu hatukusimamia hili jambo hatufanikiwi.

Mhe. Naibu Spika, naelekea kwenye afya ndani ya jimbo langu nimebahatika mimi nina hospitali ya Wilaya na serikali iliyopita Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein ametukabidhi jengo jengine la ghorofa kubwa tu. Lakini kwa kweli mpaka jana wananchi wangu wanalalamika pale hakuna dawa, wakati kipindi hicho cha Dkt. Ali Mohamed Shein suala la dawa lilikuwa halina tatizo, dawa kila wakati zipo, sasa hivi dawa hakuna kuna nini?

Mhe. Naibu Spika, wizara hii tuisimamieni ili wananchi waneemeke tukisema sisi tumalizie huku huku wananchi kule wanapata shida, dawa ile *panadol* hakuna sasa hivi huko tunakoelekea sasa hivi siko kwa sababu afya ni kitu cha kwanza.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu miundombinu kitabu hiki kimesema kuna barabara nyingi sana zitajengwa, lakini mimi nataka nimuombe Waziri wa Ujenzi na Mawasiliano aongeze kuna barabara Matemwe ambayo imepita kwenye huo uwekezaji unaoingiza serikali pesa, eneo hilo ikinyesha mvua magari pia hayapiti na huko ndio kwenye hoteli kubwa. Kwa hiyo, Mhe. Waziri wa Ujenzi na Mawasiliano hili alichukue na pia lina nafasi yake katika mwelekeo alivyokuja Mhe. Waziri Mkuu kuja kufungua njia ya Matemwe/Kijini aliizungumza hii barabara. Kwa hiyo, naomba Mhe. Waziri hapa aingize na hii barabara ya kutoka Kilimajuu mpaka Tundangaa ndani ya jimbo la Mkwajuni hizi ndio sehemu ambazo zina vitega uchumi tunatakiwa sisi tulinde, tusiunde halafu tukaachia hivyo vitu vikapotea tutakuwa hatufiki.

Mhe. Naibu Spika, kama tokea Dkt. Salmin Amour Juma alivyotawala akaleta uwekezaji huu kama tungekuwa tunasimamia hivi vitu tungekuwa tuko mbali na tuna maendeleo makubwa

sana. Lakini tunasimamia kidogo tukishatengeneza basi, sisi ni watu wa mwanzo wa kutengeneza utalii hapa, lakini sasa hivi tumeshakuwa watu wa mwisho. Mhe. Naibu Spika, twende Bara tukaangalie wenzetu wanavyopiga hatua sisi tumeshakuwa watu mwisho. Kwa hiyo, Mhe. Waziri hivi vitu vinatakiwa visimamiwe tukeshatengeneza basi kitu cha kwanza ni kusimamia.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo mimi naunga mkono hoja hii kwa nguvu zote asilimia mia moja. Ahsante sana.

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante mheshimiwa mchangiaji anayefuata ni Mhe. Zawadi Amour Nassor na ajitayarishe Mhe. Ali Abdulgullam Hussein.

**Mhe. Zawadi Amour Nassor:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii ya kuchangia hotuba ya Mwelekeo wa Hali ya Uchumi, Mpango wa Maendeleo na Bajeti kwa Mwaka 2021/22-2023/204.

Mhe. Naibu Spika, naomba kwanza nitoe salamu zangu za pole kwa familia, serikali na taifa kwa ujumla kwa msiba wa Mhe. Makamu wa Kwanza Rais, Maalim Seif Sharif Hamad lakini katika hilo naomba nikumbushe kwamba Mwenyezi Mungu anasema "*kullu nafsin dhaiqatul maut walau kana fiyburuuji mushayyadah*". Kwa hiyo, sambamba na hilo ni lazima tuseme "*innalilahi waina ilayhi rajiuun*". Tumuombe Mwenyezi Mungu aiweke peponi roho yake na Waislamu wote, lakini na sisi pia atupe kauli thabit na tuwe miongoni mwao. Baada ya hayo naomba nichukue fursa hii moja kwa moja kuelekea kwenye kitabu hiki na nimpongeze muwasilishaji wa hotuba hii kwa uwasilishaji wake mzuri na alionesha mwelekeo na moyo thabit wa kulipeleka taifa hili kule ambako wananchi wetu wana matarajio.

Mhe. Naibu Spika, katika ukurasa wake 24 aligusia kwamba kutakuwa na Tsh. milioni 49.5 ambazo zitafanyiwa miradi mbali ya maendeleo, katika hili naomba niseme kwamba tuwe makini katika kutekeleza hii miradi ambayo tuna mwelekeo nayo tutaianzisha, kwani uzoefu unaonesha miradi mingi ya maendeleo huwa ina changamoto zake na kwa kiasi fulani hainufaishi jamii au taifa kama ilivyokusudiwa. Changamoto zilizopo kwa mfano kuchelewesha miradi tujaalie mradi tulikuwa tuna mpango nao ndani ya miaka miwili ukamilike ili ulete manufaa kwa walengwa, hatima yake miradi yake miradi hiyo huchelewa kukamilika.

Kwa mfano, mradi wa Chuo cha Amali kilichopo Mtambwe na Chuo cha Amali cha Makunduchi tulitegemea ndani ya mwaka huu mwanzoni vile vyuo vianze kazi, lakini hadi sasa vyuo vile havijakamilika. Kwa hiyo, ni matarajio ya wananchi kwamba mradi unapoanza na kukamilika kwake wao huwa wanaajitayarisha kuutumia, lakini hatima yake miradi hiyo huwa inachelewa.

Mhe. Naibu Spika, changamoto nyengine miradi kukataliwa na jamii, kuna baadhi ya miradi jamii huwa wanaikataa pamoja na kwamba serikali imeshapoteza pesa nyingi. Kwa mfano, masoko yaliyojengwa kuna soko la Wingwi, kuna soko la Tumbe, kuna soko la Furaha, Ole na soko Msuka haya masoko hadi sasa hayajahamiwa. Kwa hiyo, yale malengo ya serikali na matarajio yake kwamba yale masoko yatumike pengine serikali ipate mapato pale yale masoko hadi hivi ninavyosema wananchi ni wagumu sana hayo masoko kuyahamia. Kwa hiyo, hapa hatuoni kwamba ni pesa kubwa ya serikali ambayo ilitumika, lakini sasa faida hatuoni. Je, pesa ile ya mradi kama ingelifanyiwa jambo jengine lolote pengine ingekuwa linaleta faida na tungeondoka na changamoto na lawama za wananchi. Kwa mfano, pesa

iliyotumika ingepelekewa huduma ya maji tu kusambaza *pipe* za maji kwenye baadhi ya maeneo husika pengine ingekuwa ina faida zaidi kuliko hayo matarajio yaliyowekwa.

Mhe. Naibu Spika, soko la Msuka hivi ninavyowaambia kwanza lilikuwa bovu halina viwango, na hivi sasa hilo soko halijawahi kuhamiwa hata siku moja, kinachofanyika sasa hivi ni vijana kujiingiza kwenye masuala ya ulevi na pia kufanya vitendo visivyo na maana ikiwemo ngono kwenye hayo majengo. Kwa hiyo, hapa lazima tuangalie hii pesa tutakayoitumia milioni 49 italeta faida gani kwetu, tusije tukafanya kama hivyo tulivyokosea.

Mhe. Naibu Spika, pia changamoto nyengine kwenye hii miradi ni hawa wazawa, watu wengi wanapendekeza kwamba miradi tuwape wazawa, lakini mwisho wa siku wakati mwengine huwa kuna rushwa ndani yake. Nikisema rushwa ina maana hata maana muhali ni rushwa kwa sababu tu ni ndugu tuliyempa ni ndugu yetu kwa hiyo tunaona tabu sisi kumfanyia utafiti na uchunguzi kwa sababu ni ndugu ndio anafanya vyovyote baadae aweke kitu ambacho hakitakwenda sambamba na malengo yaliyokusudiwa.

Kwa hiyo, tunavyotaka hapa nashauri kwamba pesa hii itakayotumika katika mipango ya maendeleo ya miaka hii minne, badi lazima tuhakikishe tumefanya uchunguzi wa kina kwa miradi ambayo tutaipendekeza.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo naomba nichangie kwamba suala zima la afya, katika huu mpango wa mwaka mmoja vipaumbele vya mwaka suala la afya lilitajwa kama kutajengwa tu hospitali ya Binguni. Lakini ukiachia hospitali ya Binguni ambayo itakuwa pengine ndio kubwa pia kuna vituo vyetu vya afya. Mimi nilikuwa napendekeza kwenye hii bajeti basi vingeliingizwa hivi vituo vya afya kwa sababu kuna changamoto nyingi. Mwelekeo huu haujaonesha kwamba kwa mwaka huu suala la afya tutaliangalia vipi. Kwa mfano, takriban mote kila utakapokwenda kituo cha afya hamna wauguzi pia hakuna *ratio* za madawa hamna ambapo mwenzangu alisema na kuna baadhi ya hivi vituo vyetu vya afya ni vibovu na havina hadhi. Kwa maana hiyo, bajeti hii ndani ya mwaka huu iangalie suala zima la afya wananchi wetu wanahitaji afya, elimu, maji safi na salama ndio changamoto zao huko kwenye jamii.

Kwa hiyo, suala la afya kwa mfano kituo changu cha Mkiawang'ombe kituo hicho kilianzishwa mwaka 2012 hadi leo hivi ninavyozungumza hata siku moja huko hakuna hata yule muuguzi kuna *orderly*, *orderly* huyo anaweza akatumika kuzalisha, hapo tunatayarisha vifo vya akina mama na uharibikaji wa mimba.

Mhe. Naibu Spika, kuna zana ziliingizwa humo za kufanyia uzalishaji wa huduma ya afya na mama hivyo vifaa naoma mimi baada ya miaka mitatu vitaharibika vyote viwe havifai, kwa sababu yale malengo yaliyokusudiwa vitumike havitumiki. Kwa hiyo, ninachotaka kuzungumza hapo ni kwamba bajeti iangalie suala la afya tokea ngazi ya msingi kwa sababu wananchi wetu wanahitaji wapate afya salama.

Mhe. Naibu Spika, lakini katika kipengele kingine cha 16 lilielezwa suala la elimu kuhusu maslahi ya walimu na walimu wa TuTu. Kwa hiyo, napenda niseme kwamba hapa maendeleo ni elimu na hotuba ya Mhe. Rais alipokaa na wadau wa elimu aligusia sana maslahi ya walimu na alipendekeza kwamba walimu waangaliwe kwa sababu ndio wanaozalisha hata yeye Rais alipitia kwa mwalimu na sisi humu ndani tulianzia kwa walimu. Kwa hiyo, maslahi ya mwalimu yaangaliwe kwa sababu yeye ndiye anayezalisha, yeye ndiye chemchem ya wataalamu. Kwa hiyo, tuone kwamba changamoto tena inayoikabili hii elimu ni suala zima la walimu.

Mhe. Naibu Spika, katika skuli nyingi ukipita watu wanalia na walimu, lakini ukija kuangalia kwenye wizara nyengine kuna watu hata kazi hawafanyi humo kwenye maofisi anapeleka kikombe, sahani ndio kazi yake. Lakini kule kwenye *field* ya elimu yaani hakuna mwalimu mmoja ana vipindi mpaka 50, sasa bajeti hii haijaonesha kwa mwaka huu suala la elimu kwamba wataliangalia vipi. Mimi nilikuwa napendekeza kwa mwaka huu kila mwaka hii sekta ya elimu iangaliwe kuongezewa wafanyakazi na kufanyiwa *maintenance* kwenye hayo maskuli. Kwa hiyo, walimu waajiriwe kwa lengo la kuboresha elimu yetu.

Mhe. Naibu Spika, pia kuna walimu wetu wa TuTu, wale walimu jamani wameshajitolea huu ni mwaka zaidi ya saba tayari wameshajitolea kwenye jamii zetu, wameshasomesha watoto wetu kwa sana. Kwa hiyo, kwa nini hatuoni ipo haja na wao hii bajeti ikawaangalia kuweza kuwaajiri, kwa sababu kulikuwa kuna fununu watawaajiri lakini bajeti ya mwaka huu haijataja suala zima la elimu. Nilikuwa napendekeza suala la maji safi na salama limo ambalo ndio kilio cha wengi, basi bajeti hii iangalie pia suala la afya na suala la elimu.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo naomba nimalizie kwa kipengele changu cha mwisho kwamba huu mwelekeo wa bajeti utoe vipaumbele kwa zile ahadi zilizokuwa zinawekwa na waheshimiwa wastaafu. Waheshimiwa wastaafu waliweka ahadi nyingi kwa wananchi wao, kwa hiyo na wao wanataka washukuriwe kwa sana na wananchi wao. Kwa hiyo, ahadi zilizowekwa ziwe nii vipaumbele katika mwelekeo wa miaka hii inayokuja. Kwa mfano, tunapotaja masuala ya barabara zetu za ndani kilomita 135 basi tukae tuchunguze ni barabara zipi ambazo Waheshimiwa Marais kuna barabara zina awamu zaidi ya tatu au nne. Kwa hiyo, tuseme ni barabara ipi Mhe. Rais aliyepita wa awamu ya sita nyengine pengine tokea awamu ya tano, basi tuanze na hizo hii italeta heshima ya kuwaenzi wale waasisi wetu waliopita.

Mhe. Naibu Spika, pia italeta ari kwa wananchi wetu na wataona kwamba sasa tayari kweli hii ni kasi mpya. Kwa hiyo, nasema hivyo nikiwa nina maana ya barabara yangu ya Msuka ina awamu zaidi ya nne inatajwa, barabara hiyo inaelekea kwenye bahari kuu takriban samaki wengi wa Pemba wanatokea huko Msuka lakini barabara yake haina hadhi. Mhe. Naibu Spika, hiyo barabara utaionea huruma...

**Mhe. Naibu Spika:** Mheshimiwa malizia.

**Mhe. Zawadi Amour Nassor:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nashukuru sana naunga mkono hoja hii ya hotuba ya mwelekeo wa hali ya uchumi asilimia zote Mwenyezi Mungu awabariki waandaaji lakini Mwenyezi Mungu aibariki Zanzibar. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante mheshimiwa mchangiaji anayefua ni Mhe. Ali Abdulgullam Hussein baada ya hapo ajitayarishe Mhe. Kombo Mwinyi Shehe.

**Mhe. Ali Abdulgullam Hussein:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, awali ya yote napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuweza kukutana tena katika kikao chetu cha kujadili Mwelekeo wa Hali ya Uchumi, Mpango wa Maendeleo na Bajeti kwa Mwaka 2021/22-2024/2024. Vile vile napenda nichukue nafasi hii kutoa pole kwa niaba ya wananchi wa jimbo la Jang'ombe kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuondokewa na Makamu wake wa Kwanza na vile vile natoa pole kwa wanachama wa Chama cha *ACT* Wazalendo.

Mhe. Naibu Spika, napenda kuunga mkono hoja hii kwa mipango hii mizuri ambayo inaonesha dira na dhamira ya kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ili kuhakikisha mwaka 2025 ule ushindi wa zaidi ya asilimia 76 uweze kupatikana zaidi ya ule.

Mhe. Naibu Spika, mimi nitapenda nianze kuchangia katika Shabaha na Malengo ya Uchumi kwa Mwaka 2021/2022. Shabaha na malengo kwa miaka mitatu inategemea kuwepo kwa amani na utulivu na kuwepo uwajibikaji katika kazi na uendelezaji wa kuwajengea uwezo wafanyakazi.

Mhe. Naibu Spika, kiukweli mipango yote mizuri hii inayopangwa inategemea masuala haya na mimi nishauri tu kwa upande wa serikali kuendelea kuwajengea uwezo wafanyakazi, kwani bila ya kuwajengea uwezo hivi vinavyopangwa vitashindwa kutekelezeka. Suala la uwajibikaji wahakikishe kuwa wafanyakazi wanawajibika, wanatekeleza majukumu yao ipasavyo. Na suala la kuimarisha utawala bora hili ni suala muhimu katika kuimarisha uchumi wetu, lazima misingi ya utawala bora iimarishwe, uwajibikaji usisitizwe, uwazi kwenye mikataba, ushirikishwaji wa wananchi katika kufanya maamuzi makubwa pia ni muhimu na masuala ya kuzuia rushwa hayo ndio muhimu. Kwani kwa sasa tunaona nchi yetu inaingia katika mikataba mikubwa na wanafanya makubaliano na makampuni makubwa wakati ukifanya makubaliano haya masuala ya rushwa yanachukua nafasi yake. Kwa hivyo, tuombe serikali wawe wakali kwenye kusimamia masuala ya rushwa ili tuone sasa kile ambacho kinapangwa kutekelezwa kitekelezwe kwa maslahi ya nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, niende basi katika Mwelekeo wa Mpango ambapo tumeona mpango huu una dhamira ya mageuzi ya kiuchumi. Suala la mageuzi ya kiuchumi linataka matayarisho makubwa kwa vijana wetu, kwa maana vijana wetu sasa hivi nchi yetu inaelekea kujiwekeza katika uchumi wa buluu, lakini bado tuna upungufu wa wataalamu katika eneo hili. Kwa hivyo, niishauri serikali waangalie kuwapa vipaumbele wale ambao wanahitaji kwenda kujiendeleza katika masuala haya ya mafuta na gesi, masuala ya uvuvi ili ile mikopo inayotolewa na serikali yetu kutokana na elimu ya juu waweze kupata tahfifu ili vijana wengi wahamasike katika kushiriki kwenye haya mafunzo, ili tuendane na ile kasi ya mageuzi ya kiuchumi.

Mhe. Naibu Spika, katika mpango huu vile vile mimi sijaona masuala ya michezo, katika mpango huu inaonekana wazi serikali bado haijalipa kipaumbele suala la michezo. Kwa hivyo, namtaka waziri anayehusiana na masuala ya fedha aliangalia hili. Kwa sababu katika eneo la michezo vijana wetu wengi wanapata ajira na wanaweza kuondokana na umasikini. Kwa sababu michezo inafungua ajira na michezo inahamasisha vijana kutoshiriki masuala ya vitendo viovu.

Mhe. Naibu Spika, tukienda katika vipaumbele vya taifa vya mwaka 2021, 2022, 2023 na 2024. Tumeona ni vipaumbele vizuri na vingi na vyenye tija katika uchumi wetu, lakini nishauri tu kuwa vipaumbele vingi ambavyo tumeviorodhesha vinategemea kuwa ushirikiano na sekta binafsi na makampuni ya nje.

Kama tunavyojua sasa dunia inakabiliwa na janga la *Corona* na Zanzibar kama ni kisiwa vile vile tujiandae. Kama ni kisiwa hii mipango ambayo tunategemea zaidi washirika na nchi ambazo zilizoendelea na wao wanakabiliwa na ugonjwa wa *Corona* na hali ikiwa mbaya zaidi na sisi kwetu itakuwa mbaya. Kwa hivyo, kama serikali niishauri tuandae mpango mwengine ambapo tukifeli katika mipango hii ya washirika ili tuweze kutekeleza ile mipango ambayo tumejiwekea.

Katika suala la Uwanja wa Ndege wa Pemba. Hakika huu ni mpango madhubuti kwa ajili ya utalii kwa maana tumeona Pemba kuna fursa nyingi za utalii. Kwa hivyo, niishauri serikali wawekeze nguvu zaidi katika huu uwanja ili uchumi wetu uzidi kuimarika zaidi.

Vile vile katika suala la utalii nipende pia kushauri kuwa wizara inayohusika iendelee kusisitiza, iendelee kuuhamasisha huu utalii, kwani hili ni pato ambalo tunalitegemea sana.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa wenzangu wengi wamechangia katika huu mpango na michango mizuri imetolewa na mimi vile vile napenda niungane nao kwa kuunga mkono hoja hii na ahsante nashukuru sana. *(Makofi)*

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante nashukuru. Mchangiaji anayefuata ni Mhe. Kombo Mwinyi Shehe na baada ya hapo ajitayarishe Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum.

**Mhe. Kombo Mwinyi Shehe:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa na mimi fursa hii ya kuchangia hotuba hii ya Mpango wa Hali ya Uchumi. Kwanza, nimpongeze Mhe. Waziri kwa jinsi alivyotuandalia jambo hili ni jambo jema kabisa, tumuombe Mwenyezi Mungu amuongoze ili aweze kulitekeleza jambo hili, kupanga ni jambo moja lakini kutekeleza pia ni jambo jengine.

Mhe. Naibu Spika, naomba nianze mchango wangu huu kwa kuelekea katika *page* nambari 23 kipaumbele cha saba (7) cha kitaifa. Mhe. Naibu Spika, sote tunatambua kwamba Zanzibar asilimia kubwa ya watu wetu ni vijana, takriban asilimia 50 ni vijana. Kwa hivyo, kama vijana ni wengi au ni asilimia 50 inasikitisha sana kuona kama katika mpango huu vijana wetu wamepangiwa kipaumbele kimoja tu. Kwa heshima zote nilikuwa namuomba Mhe.Waziri ajaribu kuliona hilo kufanya hivyo ni kuwawezesha vijana wetu kupata ajira zaidi na kujiondoa katika dimbwi la umasikini ambalo linawakabili kila siku.

Mhe. Naibu Spika, niendelee na mchango wangu katika eneo hilo hilo nikilenga na nikimuomba sana waziri anayehusiana na masuala ya vijana hao ahakikishe kuna zoezi hili la chaguzi za Mabaraza ya Vijana. Jambo hili kiasi fulani limekuwa na changamoto kubwa sana katika shehia zetu, mara nyingi Baraza la Vijana limekuwa na ubaguzi. Mimi niseme kwa uwazi kabisa kuna maeneo mpaka leo yanafanya chaguzi kuna watu hata zile fomu hawajawahi kuziona. Nimuombe sana Mhe. Waziri alifuatilie jambo hili na aliingilie kati ili chaguzi zinapofanyika za Mabaraza haya ziwe huru na hatimae wapatikane vijana bora kwa ajili ya kuliendeleza jukwaa hili. Jamani jukwa hili Mheshimiwa linatakiwa lijitegemee, liwe huru kabisa lisiingiliwe, lakini na pia liwakutanishe vijana wa pande zote zilizomo ndani ya nchi yetu. Nimuombe sana Mhe. Waziri nalo hili alitupie macho.

Mhe. Naibu Spika, nakwenda kwenye mchango wangu kwenye Sekta ya Afya. Sote ni mashahidi kuwa dunia imekumbwa na tatizo sugu la ugonjwa wa *Corona*, ila inanisikitisha sana kuona hadi sasa pamoja na changamoto zote hizi ambazo dunia imeikumba na jambo hili Mhe. Waziri ametueleza hapa katika kitabu chake kwenye kifungu cha 3.3 Mwenendo wa Uingiaji Watalii 2020, kwamba kutoka wageni 333,374 na kupungua hadi 102,746. Inaonekana kuna *rate* kubwa hapo chini imeshuka na imeshuka kutokana na tatizo la gonjwa hili la *Corona*. Inasikitisha kuona serikali imeshindwa kuliingiza jambo hili la afya kama ni kipaumbele cha taifa.

Mhe. Naibu Spika, kujenga hospitali ni sehemu moja lakini huduma sasa katika hilo jengo linalojengwa. Namuomba sana Mhe. Waziri aliangalie hili jambo, kwa sababu kuwepo kwake

litapelekea kuwaimarisha watu wetu kuwa na afya kamili na wakaweza kuhimili kutenda shughuli za uwajibikaji. Jamani tusidanganyane bila ya afya nadhani hakuna atakayekuja hapa, namuomba sana Mhe. Waziri katika hilo aliangalie sana.

Naomba niendelee katika mchango wangu kwenye ukurasa wa 23, kipaumbele cha nane (8), kuna suala zima la uendeshaji wa viwanda. Mheshimiwa sote tunatambua kwamba Micheweni ni eneo moja ambalo ni muhimu sana kwa suala la viwanda na ni juzi tu nadhani Mhe. Rais alikuja Micheweni kuzindua barabara ambayo itaelekea kwenye eneo la viwanda. Wakati yuko pale aliwahi kuwaahidi watu wa Micheweni kama eneo lile litakuwa ni sehemu ya viwanda, wana Micheweni nikiwemo mimi mtu wa Wilaya ya Micheweni basi tumejenga matumaini makubwa na hilo jambo. Lakini nasikitika kuona kuwa humu katika mpango huu eneo la Micheweni silioni kama limetengwa kama nalo ni eneo la viwanda.

Mhe. Naibu Spika, nimuomba sana Mhe. Waziri watu wa Wilaya ya Micheweni wana mazingira magumu sana ni ukanda ambao nadhani yeye mwenyewe anaufahamu, akisema awanyime viwanda watu wa Micheweni kwa ujumla atakuwa hajawatendea haki. Nimuombe sana ajaribu kuliangalia na hilo pia.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye ukurasa wa 22 Ujenzi wa Viwanja vya Michezo. Mhe. Naibu Spika, kujenga viwanja ni sehemu lakini hivyo viwanja kama hakuna michezo vitatumika vipi. Mhe. Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo nimuombe sana michezo Zanzibar imeshuka na ushahidi wa hili jamani ni juzi tu, tulikuwa na Kombe la Mapinduzi hapa nadhani tulipigwa. Migogoro imekithiri katika michezo. Kule Pemba sijui kukoje hakusemeki, vijana wamekataa hata kushiriki katika *league*, wamekataa kabisa kushiriki kwa migogoro, hebu tusaidiwe katika hili jambo ili michezo ikue tatizo liko wapi.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea niende kwenye eneo la kuimarisha upatikanaji wa elimu bora kwa wote. Mheshimiwa ni vyema kuimarisha elimu kwa kujenga majengo kama alivyosema Mhe. Waziri, ila naomba nimkumbushe kitu kimoja tu. Katika kujenga majengo yetu haya tusisahau pia kuyaangalia yale ambayo yamepita, kuna majengo bado yamejenga lakini hayajakamilika, tusiangalie kuimarisha kwa ajili ya kujenga mengine mapya wakati huku nyuma tumeacha mengine hayajakamilika.

Pia nimuombe sana Mhe. Waziri akumbuke kuwa kwenye serikali ya awamu iliyopita kuna skuli za sekondari kila wilaya zilijengwa, lakini bado madakhalia yake hayajakamilika. Katika hili nitaje skuli yangu ya Chwaka Tumbe ni skuli ya wilaya imejengwa kwa madhumuni ya kuwaunganisha vijana wote wa Wilaya ya Micheweni Michepuo na walale pale kwa maana ya kuwa kuwepo na dakhalia, lakini hadi sasa hivi ni jengo limekaa tu pale wanafunzi wanakuja na kurudi. Nimuombe sana Mhe. Waziri nalo pia alitupie macho.

Mhe. Naibu Spika, nikirudi tena kwenye ukurasa wa 22 Kuimarisha Utawala Bora. Ujenzi wa afisi za serikali niiombe sana serikali wakati wanapojenga majengo yetu haya ni vizuri sana wahusika wa maeneo yale wakashirikishwa katika maeneo hayo. Lakini pia tuzingatie kuna jambo muhimu sana, nitolee mfano kule Pemba. Nataka kwenda kukata leseni ya kupasisha gari kuna kitu kinaitwa *One Stop Centre*, unakwenda mawasiliano unakuja *ZRB*, unakuja Benki, nadhani wewe mtu unatembea kwa miguu hebu aangalie Mhe. Waziri hiyo *interval* mtu huyo unavyomsumbua. Eneo la mawasiliano lilipo, benki ilipo, *ZRB* ilipo. Kwa hivyo, tunapojenga majengo yetu kama haya tuzingatie jambo hili tukamilishe kila kitu kiweko pale ili yule anayekuja kuchukua ile huduma asipate tabu, umrahisishie huduma. Namuomba sana Mhe. Waziri jambo hilo aliangalie.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo machache niseme naiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja, ahsante. *(Makofi)*

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante mheshimiwa, mchangiaji anayefuata ni Dkt. Saada Mkuya Salum, baada ya hapo ataachangia Mhe. Sabiha Filfil Thani ndio atakuwa mchangiaji wetu wa mwisho.

**Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum:** Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, na mimi nachukua fursa hii kuungana na Wazanzibari na Watanzania katika kumuombea dua aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Marehemu Seif Sharif Hamad. Mwenyezi Mungu amlaze mahala pema peponi na amsamehe pale ambapo ameghafilika.

Mhe. Naibu Spika, kwa mukhtadha huu wa hoja yetu hii nachukua fursa hii vile vile kuwapa pole wanafamilia wa Wizara ya Fedha na Mipango ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Benki Kuu ya Tanzania kwa kuondokewa na wapendwa wetu aliyekuwa Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango Dkt. Servacius Beda Likwelile na asubuhi ya leo nimepata taarifa kwamba Profesa Benno Ndulu nae ametangulia mbele ya haki. Naungana nao katika kuwapa pole.

Vile vile na mimi naungana na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi katika kuchangia Hotuba ya Mwelekeo wa Hali ya Uchumi, Mpango wa Maendeleo na Bajeti kwa miaka hii ambayo imetajwa 2020/21 hadi 2023/2024. Naunga mkono hoja kwa sababu mwelekeo huu pia una mawazo ya Wajumbe wa Kamati yetu ya Bajeti na kusema ukweli tumetoka mbali, hadi tumefika hapa tumetoka mbali kweli na leo tukapata fursa ya kuipongeza na kuikubali hii hotuba ya Mhe. Waziri. Basi sina budi kuungana na yeye katika kuunga mkono hoja hii isipokuwa na mimi nikiwa kama mjumbe nina wajibu wa kikanuni vile vile kuchangia hotuba hii.

Kwanza, naanza na Sekta ya Utalii. Mhe. Naibu Spika, Sekta ya Utalii bado ni sekta kiongozi kwa mapato, lakini ni sekta kiongozi hata kwa kutoa ajira kwa vijana hapa Zanzibar. Lakini baada ya janga la *Corona* Sekta ya Utalii imebadilika *perspective* yake na *context* yake. Kwa hiyo, sisi pamoja na serikali ni lazima kuangalia upya muktadha wa Sekta ya Utalii unakwendaje. Tulikuwa tunataka kuhamasisha sana utalii, watalii waje kwa wingi na Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi imejikita huko, mpango wetu huu umejikita huko lakini *perspective* na *context* baada ya janga la *Corona* imebadilika. Kwa hiyo, *approach* ambayo tunaitumia sasa hivi lazima iendane na mazingira ambayo tuna-*operate right now*.

Sasa hivi, watalii wanaokuja sio wale watalii ambao tulikuwa tunawataka waje na waweze kufanya mambo ambayo tulikuwa tumeyaweka kwa ajili ya watalii. Sasa hivi watalii wanaokuja, wanaoingia hapa ni wale watalii ambao tunapishana nao tunapigana nao vikumbo huko barabarani, tunapanda nao daladala, tunapanda nao bodaboda. Wengine sasa wanapangisha hata nyumba sio hoteli tena, sio *rooms* tena sasa hivi ni nyumba kabisa. Kwa hivyo, watalii wa sasa hivi wanaokuja ni wale watalii ambao wanataka ku-*stay* yaani *they are here to stay definitely* lazima tuangalie utaratibu mpya wa watalii. *(Makofi)*

Lakini sio hilo tu, utamaduni mpya unakuja sasa hivi unaweza kukutana na watalii hapo wanarandaranda yaani humuelewi ni aibu kuzungumza, tumeona Mhe. Waziri ametoa waraka. Mhe. Naibu Spika, tunaomba waraka ule tupate muda angalau usomwe hapa Baraza la Wawakilishi lakini vile vile, usomwe katika vyombo vyetu vya habari kila mara kuwakumbusha tu *operators* juu ya maadili ya Zanzibar, utalii tunautaka lakini isiwe chanzo

cha kubadilisha au kuharibu maadili yetu. Kuna *products* nyingi, kuna *ethical tourism right now* ingewezekana kabisa hata tukachukua *context* ya *ethical tourism* tukaiweka hapa Zanzibar *tours operators*, sio tu tuzungumze nao hapa lakini hata huko wanakotoka tuweze ku-*connect* na *tours operators* wajue wanaokwenda Zanzibar huu ndio utamaduni wa Zanzibar hakuna kutembea utupu, hakuna kufanya mambo ya maajabu katika njia zetu.

Kwa hivyo, tunaomba kwamba Mhe. Waziri atakapokuja vile vile atwambie muktadha huu anafanya nini, tunataka tuone *action* angalau hili lionekane limepungua. Tunataka watalii lakini vile vile tuna wajibu wa ku-*preserve ethics* na *culture* yetu kama Zanzibar tuko *unique* kwa hivyo, sisi hatuwezi kuwa tunakwenda na utalii lakini ile *preservation* yetu tuliyokuwa tunayo hatuiweki, ni lazima tunapokwenda huko tujue kwamba tuna kitu ambacho sisi inatubidi tukifanye.

Jambo la pili Mhe. Naibu Spika, mpango huu wa maendeleo ni mzuri, lakini kuna jambo ambalo inawezekana likasababisha tusiweze kufikia malengo yetu kwa kiasi kikubwa, *attitude* ya kazi. Tunataka mabadiliko lakini bado tuna changamoto ya *attitude* ya kazi, nikizungumzia hapa Sekta ya Umma, Sekta ya Umma ni lazima ibadilike, Sekta ya Umma imeajiri watu wengi, sasa ukilinganisha na Sekta Binafsi, lakini kama tukienda na utaratibu huu tunaokwenda nao kwenye Sekta ya Umma tunaweza tukawa tusifike. Kuna changamoto nyingi sana tunaomba viongozi kwa maana mawaziri turudi karibu sana na watendaji wetu, kuna changamoto nyingi sana wanazokumbana nazo lakini viongozi tuwe ni sehemu ya watekelezaji tusiwe ile juu sana tuteremke chini.

Mhe. Naibu Spika, mara nyingi hapa tunakuwa tunauliza maswali na vitu vyengine unaweza ukawa unajibiwa wanasema sisi hatujui, nadhani tubadilike ili twende pamoja, hatujapata taarifa bado *problems* za miaka iliyopita tulizitatua kwa *approaches* za miaka iliyopita, *problems* zetu za leo hatutaweza kuzitatua kwa kutumia *approaches* au taratibu za miaka iliyopita. *Problems* zetu za leo ni lazima twende hatua kadhaa mbele kuweza kuzirekebisha. Tunaona yaani jinsi gani tunavyokwenda, yaani utaratibu kama umekuwa ule ule hivi wakati tuna miaka minne, mitano ya kuweza kuleta mabadiliko makubwa hapa Zanzibar. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, ni lazima Sekta ya Umma sote kwa pamoja tubadilike utendaji kazi wetu, hususan viongozi turudi chini kwa watendaji wetu tujue wanafanya nini, wana changamoto gani, pahala ambapo wamefanya vizuri tuwa-*praise* na tutabadilisha mtazamo huu.

Mhe. Naibu Spika, lakini muktadha wa ukusanyaji wa mapato. Ukusanyaji wa mapato ni jambo ambalo tumelipa kipaumbele sana. Katika hili Mhe. Naibu Spika, kuna baadhi ya taasisi zinatumia hiyo *concept* ya kuimarisha mapato ya serikali ndivyo sivyo. Mheshimiwa mwishoni wa mwezi wa Januari kulitokea malalamiko mengi sana kuhusiana na Bodi ya Vileo. Bodi ya Vileo sheria ambayo ilipitishwa na Baraza lako Tukufu hili Aprili mwaka 2020 kifungu cha 33 (1) kinasema, watakaokuwa wanaleta vileo yaani hiyo ruhusa au kibali cha wanaoleta vileo wasizidi watatu, leo tunasikia wametumia busara na sijui kwa sababu serikali inahitaji mapato Zanzibar hii wanaoleta vileo wameongezwa watatu wamekuwa sita.

Hapa leo hiyo ilivyokuwa waingizaji vileo watatu tunaiona Zanzibar hii inapokwenda, mimi mitaa ninayokaa hapo ukichukua ile *diameter* tuliyokuwa nayo pale *less than a kilometer* labda 8 au 9. Sasa leo wanakuja watendaji wanasema sisi tumechukua busara kuongeza hii kwa sababu serikali inataka mapato. Hivi aliwaambia nani serikali yetu hii inahitaji mapato ndio ifanye huo utaratibu. Utaratibu ambao ni kinyume kabisa na sheria. Baraza lako Tukufu Mhe. Naibu Spika, limetunga sheria, sheria iko *explicitly* waingizaji vileo Zanzibar

hawatozidi watatu sasa sijui hii *muscle* inatokea wapi ya kuona kwamba watendaji wanajipa mamlaka ya kutoa vibali waingizaji wengine.

Hatuwezi kulikubali hili kwa sababu hii ni *indication* kwamba Baraza hili Tukufu ambalo lilipitisha hiyo sheria kwa muktadha wa ku-*preserve* maadili ya Zanzibar limedharauliwa. Kwa hiyo, hili hatutoweza kulikubali changamoto ya mapato tunaweza tukaitatua kwa kufuata utaratibu hata tukipitisha bajeti hapa mwisho wa siku inakuja *finance deal* ambapo Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha na Mipango tunampa ruhusa aende akakusanye na akatumie. Sasa hii *approach* imetokea wapi, hii inaonesha kwamba kuna watu wana nguvu sana huko walipo. Kwa hivyo, Mheshimiwa pamoja na hili hatuwezi kuangalia utaratibu ambao utakuwa unakiuka sheria ambazo sisi Baraza la Wawakilishi tumezitunga. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, tukiendelea kwenye vipaumbele vya kitaifa mwaka 2021-2022 kuna miradi mingi imeorodheshwa. Kwanza, nataka nimwambie Mhe. Waziri atakapokuja wakati wa bajeti hapa kama hatujaona utaratibu mzima wa jinsi gani wanawake wameingizwa katika vipaumbele, maendeleo ya wanawake na jinsia kwa ujumla, basi nadhani hapa itabidi lazima tuangalie utaratibu mwengine. Kwa sababu wanawake sisi ndio tunaojenga uchumi wa nchi hii, wanawake ndio tumebeba kabisa uchumi wa nchi hii. Leo unaweza ukakuta wanasema upatikanaji wa maji upo asilimia 80 *which is fine*, lakini sasa ukiangalia upatikanaji huo wa maji tunaweza tukapima kwamba kilomita moja kutoka pale mtu anapoishi ndio maji yanapatikana.

Mhe. Naibu Spika, tukiangalia kilomita moja ya leo hapa yaani tunaweza tukafika labda Mazizini Polisi, *imagine* mama ana ndoo kichwani anatoka hapa anakwenda kutafuta maji safi na salama Mazizini Polisi anakuwaje, tunamtweza nguvu, anakosa nguvu na anakosa vile vile kuhudumia jamii. Kwa hivyo, hizi *Social Sectors including* upatikanaji wa maji safi na salama, kuimarishwa kwa afya, kuimarishwa kwa elimu lazima zimuangalie mwanamke na jinsi gani yeye anaweza ku-*contribute* katika uchumi huu.

Jambo jengine ambalo nililizungumza Mheshimiwa, Tume yetu ya Mipango iangaliwe upya ili iweze kutumia *models* ambazo zitakuwa zinatoa uhalisia wa hali ilivyo. Kwenye vipaumbele 17 Mheshimiwa kuna kipaumbele cha 13, Kuendelea na Utekelezaji wa Mradi wa Mageuzi ya Sekta ya Nishati Zanzibar *(Zanzibar Energy Sector Transformation).* Kuendelea mradi huu uliwekwa katika bajeti hii ambayo tunaendelea kumaliza hata kuanza haujaanza, huo mradi hata kuanza haujaanza ndio kwanza hata hao Benki ya Dunia hawaja-*approve* na hivi tunavyokwenda lazima kutakuwa kuna-*delay* tu. Changamoto hii ya *Corona* imeleta mabadiliko kwa kiasi kikubwa sana. Kwa hivyo, hatuwezi kuweka miradi kama hii *which have very important* lakini bado haina uhalisia tunakuza bajeti ya serikali kwa miradi ambayo hatutaweza kuitekeleza. Ni lazima Tume ya Mipango ijengewe uwezo kutengeneza *models* ambazo zitaingiza *factors* ambazo zitakuwa zinaathiri moja kwa moja utekelezaji wa mipango ya maendeleo.

Huu ni mradi mmoja lakini kuna miradi mingine haijaanza na hapa ndio maana waheshimiwa wakisimama wanasema, bajeti ya maendeleo haijatekelezwa sio kuwa haijatekelezwa kwa sababu miradi inayoingizwa inakuwa ni miradi ambayo wala kuanza haijaanza, tunaingiza tunaitia katika hesabu bajeti hiyo tunakwenda trilioni 1, bilioni 500 lakini ndani yake kuna miradi ambayo hatujaianza kabisa na haiwezi hata kutekelezwa.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine la mwisho ni kuhusiana na masuala mazima ya Sekta Mtambuka hususan udhalilishaji, tulizungumza udhalilishaji wa wanawake na watoto ni

Sekta Mtambuka, hili ni lazima tuwe tunaliona katika bajeti likijitokeza wazi wazi jinsi gani *sectors* zinajikinga au zimeweka kipaumbele au mkazo kwa masuala kama haya. Yapo haya hata maofisini kwetu yanatokea tuone hizi *sectors* zinafanya nini kabisa katika muktadha huu. Tunamshukuru sana Mhe. Rais kuona amesimama kidete kuhakikisha kwamba hizi mahakama zinazosimamia hususan masuala haya ya kupinga udhalilishaji zinafanya kazi na amezipa kipaumbele.

Lakini changamoto ambayo naiona ile itakuwa ni *final* kuingia mahakamani, lakini huku nyuma kutakuwa na *process* nyingi sana, waende polisi sijui wakachukue *PF3*, waende *DNA* yaani ni *process* nyingi. Upande wangu binafsi nashauri kuwe kuna taasisi moja ambayo itasimama katika kuratibu hizi *process* ambazo muathirika inabidi apitie kabla ya kufikia pale mahakamani kuwe kuna *One Stop Center*, kama vile ambavyo tumeanzisha Kamisheni ya Madawa ya Kulevya, Kamisheni ya Ukimwi, Kamisheni ya Maafa kwa sababu hizi zilikuwa ni changamoto ambazo zinaathiri uchumi.

Kwa hivyo, masuala haya ya udhalilishaji yaandaliwe taasisi yake ambayo itasimamia na itaratibu zile *process* ambazo muathirika anapitia kabla ya kwenda mahakamani kwa sababu hizi ndizo ambazo zinasababisha watu wasiende kuripoti. Hizi *process* wanazopitia huu urasimu ndio unaosababisha watu kuchoka na urasimu huu ndio unasababisha watu kuendelea kufanya hivi vitendo. Lakini tukiwa tuna taasisi moja ambayo itasimama imara kuona kwamba inaratibu haya masuala kabla ya kwenda mahakamani, basi nadhani tutakuwa tunafanya jambo la busara na tutasaidia sana kwenye hilo. Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika na naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante sana Mheshimiwa, mchangiaji wetu wa mwisho kwa upande wa wajumbe atakuwa ni Mhe. Sabiha Filfil Thani. Mheshimiwa karibu.

**Mhe. Sabiha Filfil Thani:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma kutujaalia siku ya leo kuamka tukiwa wazima na wenye afya njema. Napenda kutoa pole kwa familia na wanachama wote wa *ACT* Wazalendo na wananchi wote wa Zanzibar kufuatia kifo cha Makamu wa Kwanza wa Rais, Marehemu Mhe. Seif Sharif Hamad Mwenyezi Mungu amlaze mahala pema peponi. Amin. Na sisi Mwenyezi Mungu atupe hatma iliyokuwa njema.

Pia napenda kumpongeza Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha na Mipango na watendaji wake wote walioshirikiana kwa namna moja au nyengine kuweza kukamilisha Mwelekeo wa Hali ya Uchumi, Mpango wa Maendeleo na Bajeti kwa mwaka 2021/2022 - 2023/2024. Sambamba na hilo, napenda kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum kwa uwasilishaji wake wa Taarifa ya Kamati ya Bajeti kwa umahiri mkubwa. Hongera UWAWAZA.

Mhe. Naibu Spika, niendelee kuchangia ukurasa wa 5 kuna kipengele cha pili hiki ambacho kinahusu usafirishaji wa bidhaa nchi za nje. Kuna huu ununuzi wa zao la karafuu katika kipindi cha mwaka 2019 zilinunuliwa karafuu tani 1,638.5 na kwa mwaka 2020 ni tani 206.5 kuna tofauti kubwa ya uzalishaji, sasa hii sijui kama ni mzao ulikuwa mdogo au vipi. Lakini nimepata hitilafu kidogo na mshangao mkubwa juzi nimemuona Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini akishirikiana na vyombo vyetu vya ulinzi na usalama wakamkamata mwananchi ambaye alikuwa na magunia zaidi ya 40 ya karafuu. Tunaomba wananchi washirikiane na vyombo vya ulinzi kusaidia kuwakamata hawa wanaohujumu uchumi, ili wananchi waweze kuzalisha zaidi na kuweza kupata manufaa wao pamoja na serikali.

Mhe. Naibu Spika, pia napenda kuchangia kwenye kipengele hichi hichi tumezalisha tani 206.5 lakini tumesafirisha tani 946. Kwa hivyo, uzalishaji umepungua kuliko usafirishaji. Je, kulikuwa kuna *stock* ambayo ilikosa soko ilikuwa imebakia hapa, kwa hiyo mwaka huu ikasafirishwa nilikuwa naomba kuelimishwa hilo. Tunaomba Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kuongeza jitihada ya uzalishaji wa miche ya mikarafuu na tunaomba viongozi na wataalam wa kilimo waendelee kuhamasisha wananchi wetu wapande mikarafuu kwa wingi na waihudumie, ili iweze kuzalisha karafuu kwa wingi na kuweza kuongeza pato la taifa. Karafuu zimewatoa watu sana kimaisha kuna watu wamejenga nyumba, wamesomesha watoto wao, wamekwenda Makka na kadhalika. Tuimarishe zao hili kwa faida ya wananchi na taifa kwa jumla.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapa naendelea katika ukurasa huu wa tano kuna kipengele hichi cha MKUZA III utekelezaji wa MKUZA III kwa mwaka 2019-2020 ni wananchi wanaoishi kwenye umasikini waliokithiri 25.7. Je, serikali ina mpango gani wa kuondosha umasikini uliokithiri kufikia asilimia 10 kwa mwaka 2021 kama ulivyojipangia.

Mhe. Naibu Spika, nataka kuchangia hapa ukurasa wa 8 kuna bilioni 61 ikiwa ni kama sehemu ya marejesho ya ujenzi wa *Terminal III* kutoka *Exim Bank.* Miongoni mwa asasi za mapato ya serikali ni bilioni 61 ikiwa ni sehemu ya marejesho ya ujenzi wa *Terminal III* kutoka *Exim Bank* hakuna sehemu yoyote ambayo imeonekana fedha hizi zimerejeshwa. Kuna tatizo gani lililosababisha kuwasilisha fedha hizi.

Mhe. Naibu Spika, naendelea kuchangia ukurasa wa 10 na 11 utekelezaji wa mapato na matumizi wa miezi 6. Ukiangalia katika kitabu hichi hapa mapato yamezidi kuliko matumizi. Mwenzangu alisema yapo sawa, hayapo sawa. Mapato ni kidogo, matumizi ni mengi. Je, inakuwaje unatumia pesa nyingi kuliko unavyozipata. Hapo nilikuwa kidogo nataka niwekwe sawa.

Mhe. Naibu Spika, naendelea na ukurasa wa 7 kipengele cha 9 kuna ujenzi wa mji mpya Kwahani. Mwenzangu hapa alizungumza, mwaka jana Mhe. Rais Dkt. Ali Mohamed Shein alipokwenda kuzindua nyumba za kisasa hizi za Kwahani alisema mji ule ni endelevu. Ule ni ujenzi wa *phase* ya kwanza tu, kutakuja *phase* ya pili, *phase* ya tatu, alimradi ule mji wote mpaka Kwaalinato kule utakuwa ni mji wa kisasa. Wananchi walijenga matumaini makubwa kuona mji wao utaendelezwa uwe wa kisasa.

Mhe. Naibu Spika, sasa ninapoangalia katika hivi vipaumbele huu ujenzi hapa siuoni, haukupewa kipaumbele. Je, pale ndio umefikia mwisho au kuna mpango gani ambao serikali umeupanga lakini hapa katika vipaumbele haukujionesha. Naomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa anijulishe kidogo.

Mhe. Naibu Spika, jengine ni ujenzi wa Barabara ya Jozani - Charawe - Ukongoroni sijaona barabara hii katika vitu vya vipaumbele. Barabara hii imetolewa ahadi na Mhe. Rais tokea Mhe. Rais Amani Abeid Karume kwamba ataijenga. Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein alisema yeye ataijenga barabara hii kabla hajaondoka madarakani.

Mhe. Naibu Spika, tunapozungumza hii barabara imejengwa kwa kiwango cha lami kama kilomita moja tu, baada ya hapo, kilichofuatia hapo magari na vifaa vile vyote vimeondoshwa. Je, serikali ina mpango gani wa kuimaliza barabara hii. Na tuendelee kuziheshimu ahadi za viongozi hasa pale ambapo ule mradi tayari umeshaanza, lakini kati

kati ya mradi unakatizwa. Matokeo yake vifaa vile vimeondoshwa vinakwenda kufanya mambo mengine.

Mhe. Naibu Spika, ni matarajio yetu kasi ya ukuaji wa pato la taifa utaongezeka ili bajeti hii iweze kutekelezeka. Sambamba na hilo, kuweza kudhibiti kasi ya mfumko wa bei ili tuweze kufikia lengo tulilokusudia.

Mhe. Naibu Spika, napenda kuwapongeza mawaziri walioteuliwa kusimamia wizara. Tunaahidi tutashirikiana nao katika kutekeleza majukumu haya ya taifa. Nawaomba waongeze kasi ya ufuatiliji na usimamizi ili waende sambamba na kasi ya Mhe. Rais. “Yajayo ni neema tupu”. Baada ya marekebisho haya naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante nakushukuru Mheshimiwa. Sasa Waheshimiwa Wajumbe tunaanza na Waheshimiwa Mawaziri. Nitaanza na Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, atafuata Mhe. Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, baada ya hapo tutakwenda na Mhe. Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale. Baada ya hapo nitaelezea zaidi. Mheshimiwa karibu.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, awali ya yote na mimi nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa hii leo na mimi niweze kuchangia mpango huu wa Hotuba ya Mwelekeo wa Hali ya Uchumi, Mpango wa Maendeleo na Bajeti kwa mwaka 2021/2022 na 2023/2024.

Mhe. Naibu Spika, pia niungane na Wajumbe wote wa Baraza lako kumpa pole Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na Wazanzibari wote kwa ujumla na Watanzania juu ya msiba uliotukuta wa Kiongozi wetu mpendwa, Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar lakini pia kuwapa pole wanachama wa chama chake, Chama cha *ACT*.

Mhe. Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia kumshukuru na kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa jinsi alivyoweza kutuunganisha Wazanzibari sote kwa ujumla pamoja na kumpa heshima za kipekee na zote kwa upande wa serikali yake pamoja na vyombo vya ulinzi na usalama katika kumsindikiza marehemu katika safari ya mwisho. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema. Amin.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo, sasa niende katika mchango wangu juu wa suala zima. Kwanza, ningependa niyaseme mambo machache/kadhaa juu ya suala zima katika upande wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Katika programu ya miradi tunayotarajia kutekeleza katika kipindi cha mwaka 2021-2022 mipango yetu itajikita katika programu ya kuimarisha miundombinu ya elimu. Tumejipanga kuimarisha miundombinu ya sekta hii ya elimu kiujumla pamoja na kuwawezesha wananchi katika kuwapatia elimu bora na yenye tija.

Mhe. Naibu Spika, katika uimarishaji wa elimu ya maandalizi, tutahakikisha watoto wote ambao tunakusudia wenye umri wa kuanza skuli kwa ngazi za maandalizi na kwendea juu basi wanapatiwa masomo. Halikadhalika, katika uimarishaji wa elimu ya msingi pamoja na elimu ya lazima, elimu mbadala na elimu ya juu, msimamo wa serikali pamoja na wizara yetu itakuwa ni hayo hayo.

Mhe. Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia kumshukuru na kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar kwa mkutano maalum alipoita wadau katika sekta ya elimu waweze kutoa mawazo yao, fikra zao, lakini pia ile hamu ambayo walikuwa nayo ya kuona kwamba kunafanyika mapinduzi ya kipekee katika sekta ya elimu kwa upande wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, kipimo cha elimu kwa upande wa serikali au wizara tunapochukua sisi, tunaangalia mbali ya ufaulu, lakini pia tunaangalia jinsi gani katika elimu ya juu vijana wetu wataweza pia kujikita kuweza kujiajiri, lakini pia kujiendeleza katika maisha yao na katika kutumikia taifa lao.

Mhe. Naibu Spika, moja katika channgamoto ambayo tumeiona iliyozungumziwa ndani ya Baraza hili kwa tafsiri ya kipekee au pamoja na wadau ni juu ya elimu ya msingi na kufanya mabadiliko. Kwa sasa kwa upande wa wizara tumekamilisha na tuna mpango wa kuleta mabadiliko makubwa katika elimu na kwa kupitia sera yetu ya elimu. Lakini pia sasa hivi tunaifanyia marekebisho Sheria ya Elimu ya Mwaka 1982 ili itakapokuwa tayari iweze kupelekwa kwa wadau, lakini kuleta katika Baraza lako hili ili iweze kusomwa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waweze kuichangia.

Mhe. Naibu Spika, ni muhimu tunapozungumzia suala zima la elimu katika mabadiliko, hatuwezi kufanya mabadiliko ikiwa sera yetu sisi haijakamilika. Sera ndio itakayoweza kutuongoza, sera ndio itakuwa msingi wa mapinduzi ya elimu yetu kwa upande wa Zanzibar. Tumesikia wengi wanazungumza suala la umri, kwamba wanataka umri wa mtoto anapoanza na katika kuendelea uwe angalau mtoto akimaliza elimu ya sekondari awe ana ufahamu wa kutosha.

Mhe. Naibu Spika, wadau wamechangia kuhusu masuala ya masomo. Wengine wanasema masomo ni mengi, wengine wanazungumza masomo mengine pia yawe katika lugha. Kwa hivyo, yote haya tutayaangalia katika sera na mitaala yetu huko tunakokwenda.

Pia, wengine wamezungumzia umri wa kumaliza darasa la sita, kwamba mtoto anamaliza darasa la sita anakuwa bado ni mdogo, tuangalie mtoto amalize darasa la saba kwa upande wa msingi. Kwa hiyo, haya yote tutayazingatia na kabla ya sera kuletwa katika Baraza patafanyika semina maalum ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waweze kuifahamu na wao pia waichangie baada ya hatua ambazo tumepita.

Mhe. Naibu Spika, cha msingi yale yote ambayo yamekuwa kiu ya waheshimiwa pamoja na wananchi wa Zanzibar jibu lake litakuwepo katika sera ambayo tutaileta ili mabadiliko haya yakawepo katika elimu.

Mhe. Naibu Spika, katika suala la *vocational training*. Elimu hii ya kuweza kuwasaidia watoto wetu. Pamekuwa na muamko kwamba wanafunzi wanaokwenda kusoma katika *vocational training* ni wale ambao pengine ufaulu wao unakuwa ni wastani au ufaulu pia uliokuwa si wa kuridhisha.

Mhe. Naibu Spika, kupitia Baraza lako tukufu leo hili pamoja na Waheshinmiwa Wajumbe, niwaambie kwamba suala la *vocational training* ni suala la kuweza kuwasaidia vijana wetu mbali ya kujiajiri, lakini pia katika hatua nzima ya kuweza kujiendeleza. Yule ambaye ataweza kujiajiri na akamaliza masomo yake ikiwa ni *mechanical engineering*, *electrical engineering* na maeneo mengine, anapojiajiri na kufungua kampuni yake, hatua zake, mabadiliko yake kimaisha na matunda yanakuwa ni kwa haraka zaidi.

Mhe. Naibu Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kipindi hichi cha miaka mitano kwa kupitia ilani pamoja na hotuba ya Mhe. Rais alipokuja hapa kuzindua Baraza amezungumza mengi sana, hasa katika suala zima la uchumi wa buluu na fursa zitakazokuwepo. Sisi kwa upande wa elimu sasa tunajipanga katika yale yote ambayo tunaweza kuwasaidia wadau wale waliokuwemo ambao wanategemea kuingia katika sekta tofauti.

Mhe. Naibu Spika, tunapozungumza suala la kwenye vyuo vyetu vya *vocational training* tayari tuna vyuo viwili vipya Daya cha upande wa Pemba na Makunduchi. Tunategemea kipindi chochote sasa hivi, katika mwezi wa pili masomo yataanza. Tupo katika utaratibu wa kuhakiki wafanyakazi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, niseme tu kwamba pia kwa upande wa mpango wa serikali na wizara yetu, tuna mpango wa kujenga chuo kama hiki kwa upande wa Mkoa wa Mjini Magharibi ili katika mikoa yetu ya Unguja na Pemba sasa tuwe tuna vyuo maalum vizuri na vya kisasa.

Mhe. Naibu Spika, pia niombe kwa kupitia Baraza lako, shilingi ina pande mbili, wakati serikali inapozungumzia suala la elimu bure, afya bure, maji bure lakini bure hii tunayoizungumza ni kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kupitia bajeti yake inalipia gharama zote hizi kwa ajili ya wananchi kupata hii huduma. Na hakuna budi kwamba Wazanzibari na wananchi wote kwa ujumla, walinde katika maeneo yote haya. Kwa mfano, ikiwa ni miundombinu ya kwenye maji lakini pia katika sekta hii ya elimu, tunachoomba ni kwamba ushiriki wa wazazi pamoja na walezi uwe ni jambo la msingi.

Mhe. Naibu Spika, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wananchi wamekuwa wakali sana. Ninaposema wakali maana yake wanataka kuona mabadiliko haya, lakini ni jukumu letu sisi sote tukiwa wazazi kuhakikisha kwamba watoto wetu wanaporudi nyumbani basi angalau wanapata muda wa kudurusu. Haiwezekani mtoto begi la skuli anapotoka nalo, akitokana nalo asubuhi, akirudi nalo nyumbani mchana saa 7:00 au 8:00 linabakia vile vile mpaka siku ya pili asubuhi. Malalamiko haya tunayapata kutoka kwa walimu pamoja na watu mtaani na wazee.

Mhe. Naibu Spika, mimi niombe tu kwamba katika skuli hizi hizi ambazo tunaona wanafunzi tena wengine katika familia wazazi wao wenye hali duni ya kimaisha, lakini unakuta mtoto *performance* yake inakuwa ni nzuri zaidi. Lakini skuli hiyo hiyo kuna mzazi ambaye mazingira yake ya kimaslahi na kifedha katika maisha yake ni mazuri zaidi. Kwa hivyo, lazima wazazi na walezi washiriki katika malezi ya watoto pamoja na kuhakikisha kwamba watoto wao wanakuwa wanadurusu. Mtoto hataweza kupasi katika masomo yake na aka-*perform* vizuri ikiwa mzazi atamuachia mkono.

Mhe. Naibu Spika, leo mitaani tunaona walimu wanahangaika, wazazi wanapelekewa barua lakini unakuta wakati mwengine mzazi hata kufika skuli hafiki. Kamati za Skuli tunazishajihisha kusimamia na niwapongeze sana kamati zetu za skuli na hao walimu ambao pia wana mapungufu kwa kazi nzuri wanayofanya. Kwa hivyo, ni jambo la msingi sana pale ambapo mzazi anapelekewa barua kufuatilia mwenendo wa mtoto wake, basi ni muhimu sana kuhakikisha kwamba anafika.

Mhe. Naibu Spika, hasa nitoe wito kwa kina baba. Hata ukienda katika mahafali ya wanafunzi wetu hawa, mara nyingi utakuta wakina mama ndio wanaoshiriki, kina baba huwaoni. Niseme tu kwamba kupitia katika mambo yote mazuri ambayo kina baba

wanafanya, hili moja kidogo tunatakiwa tukazane ili tuhakikishe katika masomo ya watoto wetu tunakwenda vizuri.

Mhe. Naibu Spika, pia pamezungumziwa kuhusu walimu wa Tutu. Hawa tayari tunawalipia lakini pamezungumzwa katika kuboresha mfumo wa malipo yao. Hili tutalisimamia na mpango mkuu. Tayari wizara tumeandaa mpango wetu baada ya Mhe. Rais kutuagiza katika miaka tunayokwenda. Lakini kama tunavyofahamu mapungufu yote tuliyokuwa nayo katika masuala ya kuboresha maslahi ya walimu pamoja na kuanza kuleta mapinduzi katika kuongoza kujenga maskuli ya ghorofa na mengineyo, pamoja na kuboresha maabara, lazima tutambue kwamba uchumi wa nchi pamoja na wa dunia unapita katika nafasi ngumu hasa katika huu ugonjwa wa *COVID 19.*

Mhe. Naibu Spika, sisi Wazanzibari tumebahatika angalau hivi sasa bado tupo katika hali nzuri. Kuna nchi duniani zipo vibaya sana, akiba yao wameshaimaliza, hawajui wanaelekea wapi na wengine wamefikia pahala kwamba hata serikali zao sasa katika kukopa wanafikia katika ile nafasi ya mwisho. Kwa hiyo, sisi bado serikali yetu ipo katika hali nzuri na tujipongeze na tumshukuru Mwenyezi Mungu kwamba bado tunakwenda vizuri. Ninaamini Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha na Mipango atakapokuja hapa atalifafanua vizuri hili, jinsi gani tulivyojipanga katika suala la kifedha kusimamia maslahi ya Wazanzibari.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa sekta ya afya naomba nigusie tu kidogo, pamezungumzwa sana. Lakini niseme tu kwamba moja ambalo Mhe. Rais amelikazania nalo ni suala la bima ya afya. Bima ya afya itakuwa ni mkombozi wetu sisi Wazanzibari, lakini pia kuhakikisha kwamba katika vitendea kazi na huduma inayopatikana katika hospitali zetu pamoja na Hospitali kuu, Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja, hospitali zetu za wilaya na mkoa pamoja na vituo vyetu vya afya.

Mhe. Naibu Spika, changamoto katika kila nchi, suala la elimu na afya linamgusa kila mwananchi. Mimi kupitia Baraza lako Mhe. Naibu Spika, niwapongeze sana Waheshimiwa Wawakilishi kwa michango yao waliyotupa, kwa lugha ya Kiingereza tunasema *we value it.* Tunawashukuru kwa sababu tunaamini ndani ya serikali hii moja ya muongozo ni kutushauri Waheshimiwa Wawakilishi kwa sababu wao tayari wanaingia kule katika mzizi, wanafahamu kiu ya wananchi, wanafahamu jinsi gani ya kuweza kuishauri serikali ili ipeleke zile huduma ambazo tunazitaka. Kwa hiyo, kwa upande wa sekta ya afya, mimi ninaamini bima ya afya itakuwa ndio dawa moja kubwa katika kutusaidia.

Mhe. Naibu Spika, halikadhalika pia pamezungumziwa utaratibu mzima wa madawa. Nimefanya ziara katika bohari yetu kuu ya madawa, nimeona jinsi utaratibu wa dawa unavyopelekwa, wanatumia *system* nzuri kabisa ya kulipia ya madawa. Lakini changamoto iliyokuwepo ni kwamba tunachokitaka katika mfumo ambao tumewaelekeza dawa inapotoka katika ghala ya madawa au bohari ya madawa mpaka inafika katika kituo cha afya yule ambaye atafaidika/atatumia basi ajulikane ili kuondosha udanganyifu na kusema dawa zimepotea, zimeibiwa au hazikufika pahala panapostahiki. Ni jambo la msingi sana kwa sababu serikali inatumia fedha nyingi sana. Kwa hiyo, ni muhimu sisi kwa upande wetu kutambua.

Mhe. Naibu Spika, pia tuna changamoto katika maeneo tofauti, lakini ninaamini katika mageuzi yote katika awamu hii ambayo inaongozwa na Mhe. Rais Dkt. Hussein Ali Mwinyi basi maeneo haya tutaweza kubadilisha. Mimi niwaombe Waheshimiwa Wawakilishi katika bajeti kuu ya serikali itakapokuja...

**Mhe. Naibu Spika:** Mheshimiwa malizia.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, katika bajeti kuu ya serikali basi mambo yatakwenda vizuri na tutaweza kuwasaidia na kuweza kutoa ile huduma ambayo inastahiki.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie tu, la mwisho ni jambo ambalo linaguswa au linazungumziwa mtaani pamoja na Baraza lako ni suala zima la ugatuzi kwenye suala la elimu na afya juu ya vituo vyetu na huduma ambazo zinapatikana.

Mhe. Naibu Spika, katika mfumo wowote unapoleta mabadiliko panakuwa na changamoto. Kwa hiyo, sisi kwa sasa tunafanya tathmini, tutazidi kuliangalia baadae tutakuja na majibu rasmi kwa upande wa serikali na wizara zetu mbili ili kuhakikisha kwamba kila tunachokifanya kinakwenda katika mstari.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo nikushukuru sana kwa kunipa nafasi kutoa mchango wangu. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Tunguu naunga mkono hoja asilimia mia juu ya mia. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante. Waheshimiwa Mawaziri ambao nitawataja hapa kwa ajili ya kuchangia na wao nitawapa dakika kumi kumi ili tumpe nafasi nzuri kabisa Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha na Mipango aweze kujibu hoja na kufanya majumuisho.

Kwa hiyo, muda tunao lakini inabidi tuutumie vizuri. Naona na vile vile najua Mheshimiwa ametumia muda mrefu kidogo kwa sababu alikuwa na wizara mbili Mhe. Simai Mohammed Said, ndio maana ametumia muda mrefu zaidi, tunaendelea.

Waheshimiwa Wajumbe sasa mchangiaji anayefuata atakuwa ni Mhe. Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, baada ya hapo anafuata Mhe. Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale na ajitayarishe Mhe. Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo.

**Mhe. Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:** Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kuweza kunijaalia nikiwa katika hali ya uzima na afya katika kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Nchi (OR) Fedha na Mipango.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nalipa shukrani Baraza lako tukufu hili la Awamu ya Nane kwa michango yao katika hotuba hii ya Fedha.

Lakini pia nawashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Paje kwa kuweza kunichagua kuwa mimi ndiye Mwakilishi wao.

Mhe. Naibu Spika, nampongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuchaguliwa kuongoza katika awamu hii ya nane.

Lakini pia natoa pole kwa Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais, Maalim Seif Sharif Hamad kwa kufariki kwake Mungu aweze kumpa nafuu katika malazi yake mema. Amin

Lakini vile vile Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Mwelekeo wa Hali ya Uchumi, Mpango wa Maendeleo na Bajeti kwa mwaka

2021/2022 - 2023/2024. Nimpongeze mwasilishaji Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha na Mipango kwa umakini wake katika ufanyaji wake wa kazi hizi za fedha.

Mhe. Naibu Spika, nianze na ukurasa wa 3 ambao ni kupunguza kiwango cha kodi ya *VAT* kwa kweli kutoka 18 mpaka 15. Lakini vifaa vya uvuvi vile vile ni kutoka 18 mpaka 15. Wafanyabiashara wadogo wadogo ada za usajili na uwekezaji hii kwa kweli ni motisha kubwa ambayo ni kivutio kikubwa katika uwekezaji wa nchi yetu.

Tukiendelea katika ukurasa wa 7 Kuimarisha Ulinzi na Usalama kwa kweli hili ni jambo kubwa sana litatufanya kwamba wawekezaji wetu waweze kuvutiwa kuja katika nchi kwa sababu bila ya kuwa na ulinzi na usalama katika nchi hakiwezi kwenda kitu chochote ambacho kitaleta manufaa katika taifa hili.

Mhe. Naibu Spika, vipaumbele vya kitaifa kwa mwaka 2021/22 kwa kweli vipo *smart* sana ambavyo vina sifa na vimewekwa kwa wakati wake na mambo yote ambayo yanahitajika katika ufanyaji wa hizi shughuli.

Vile vile Mhe. Naibu Spika, katika kuimarisha Sekta za Uchumi (c) ilieleza kwamba kuna mambo ya kueleza na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji ambayo imechangiwa na Mhe. Bihindi Hamad Khamis, Mhe. Panya Ali Abdalla, Mhe. Issa Haji Ussi, Mhe. Suleiman Haroub Suleiman na Mhe. Haji Shaaban Waziri.

Mhe. Naibu Spika, kama tunavyofahamu kilimo hichi kina jumla ya hekta 810 kati ya 8,521 zimeendelezwa kwa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji na kunufaisha wakulima wa mpunga wapatao 8,000. Sambamba na kuongeza kwa tija ya uzalishaji ambayo tunategemea kukamilika kwa miundombinu hii wananchi wataongeza tani za uzalishaji ambazo mwanzoni walikuwa wanapata tani 100.3 lakini ikimalizika miundombinu hii watapata 4.5 kwa hekta moja.

Mhe. Naibu Spika, uchukuaji wa hatua maalum za kusaidia zao la karafuu kwa kweli hili limechagiwa sana na Mhe. Juma  Ali Khatib, Mhe. Hassan Khamis Hafidh, Mhe. Yussuf Hassan Iddi, Mhe. Harusi Said Suleiman na Mhe. Sabiha Filfil Thani.

Mhe. Naibu Spika, wizara yangu itaendelea kuliimarisha zao la karafuu kwa kuwapa mikopo wakulima na kutafuta masoko zaidi ya zao hili duniani kote. Wizara yangu pia tutaendelea na kuzalisha miche ya mikarafuu na kuwapatia wakulima bila ya malipo. Hili litatusaidia wakulima wote waweze kusaidia katika upandaji na kuweza kuinua kipato chao na kipato cha taifa.

Mhe. Naibu Spika, tunayo idara ya uhakika ya chakula, hichi ni kitengo cha uhifadhi wa chakula na tahadhari ya mapema ambayo tunasema ni *early warning* inatoa taarifa za mambo ambayo yatakuja baadae, ili kuhakikisha kwamba tunaweka akiba kwa ajili ya kuweza kujikimu.

Kwa kumalizia pia namshukuru Mhe. Sulubu Kidongo Amour kwa kuchangia suala la zao la tangawizi na manjano katika kuongeza uchumi wa nchi yetu. Wizara yangu sasa inatilia mkazo katika mazao haya iwe ni mbadala wa zao la karafuu. Hivyo, tutaanza kutoa elimu zaidi ili wanancni waendelee na kuendeleza mazao haya ili serikali iweze kujiongezea uchumi wa taifa letu hili.

Kwa kumalizia nawashukuru wote waliochangia hotuba hii. Lakini nawashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Paje na pia namshukuru Rais wa Zanzibar kwa kazi kubwa anazozifanya kwa maslahi ya Wazanzibari.

Mhe. Naibu Spika, mwisho, naikubali hotuba hii ya Mwelekeo wa Hali ya Uchumi, Mpango wa Maendeleo na Bajeti kwa mwaka 2021-2024 kwa asilimia mia moja. Ahsante Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

**Mhe. Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nichukue fursa hii kwa kunipa nafasi na mimi ya kuchangia machache katika hotuba hii ya Muelekeo wa Hali ya Uchumi, Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya mwaka 2021/2022 na 2023/2024.

Mhe. Naibu Spika, kwanza napenda kuchukua nafasi hii pia kutoa mkono wa pole kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Serikali yake kwa kuondokewa na Makamu wa Kwanza wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Maalim Seif Sharif Hamad. Mwenyezi Mungu amsamehe makosa yake yeye na sisi na amjaalie awe miongoni mwa waja wake wema. Amin.

Lakini pia nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha na Mipango kwa uwasilishaji wake mzuri wa hotuba ya Muelekeo wa Uchumi na Mpango mzuri ambao umeelezwa katika hotuba hii.

Mhe. Naibu spika, naomba niende moja kwa moja katika kutoa ufafanuzi baadhi ya mambo ambapo Wajumbe wengi wamechangia. Lakini kabla ya kutoa ufafanuzi naomba pia niwapongeze wachangiaji wote wa Baraza hili tukufu ambao wamechangia hotuba hii na nikitizama katika rikodi zangu karibuni asilimia thamanini ya wote waliochangia basi wamegusa Sekta ya Utalii. Ni kuonesha umuhimu wa sekta hii na kuwa kweli sote tunakubali kuwa utalii ni sekta mama na ndio tegemeo letu ambalo tunategemea kama nchi.

Kwa hiyo, niwashukuru na niwaambie tu nimechukua maoni yao yale ambayo yapo kwenye uwezo wa kuyafanyia kazi tumeyafanyia na yale ambayo kama ushauri tumeyachukua na changamoto na baadhi ya mambo nitatolea ufafanuzi.

Mhe. Naibu Spika, nikianza katika vipaumbele wachangiaji wengi walichangia kuwa katika hotuba hii mwelekeo huu haikuonesha vipaumbele vya Sekta ya Utalii na ukizingatia ni sekta mama. Kwa hiyo, katika ukurasa wa 24 kipengele cha 12 Kuanza Utekelezaji wa Mpango Shirikishi wa Kukuza Uchumi Zanzibar *(Boosting Inclusive Growth for Zanzibar)* ambayo tunaita *BIG -Z*. Kwa hiyo, katika kipengele hichi tunazo *component* za utalii ambazo zina miradi mikubwa tumekusudia kama serikali kuifanyia kazi kwa mwaka huu 2021/2022. Kwa hiyo, wale ambao walikuwa wanasema kuwa Sekta ya Utalii imesahaulika naomba kwa ajili ya hadidu rejea kipengele hicho tunayo miradi mikubwa ambayo itakuwa inajumuisha ujenzi wa kuboresha vivutio vyetu vya utalii lakini na kujenga vituo mbali mbali vya kiutalii kwa ajili ya wananchi wetu kupata kuuza bidhaa zao lakini pia na kupata kufanya shughuli zao za kitalii. Hiyo ni kitu kimoja.

Lakini pia katika vipaumbele hivi hivi vya serikali vya kitaifa vya mwaka 2021/2022 katika mashirikiano ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi kuna ujenzi wa Kituo cha Biashara na Mikutano ya Kitaifa Nyamanzi. Hichi ukitizama kimewekwa huku lakini pia ni ujenzi ambao unahusiana na Sekta ya Utalii kwa sababu *convention center* itakuwa wageni mbali mbali na mikutano mbali mbali ya kitaifa itakuwa inafanyika. Kwa hiyo, moja kwa moja Sekta ya

Kitalii itakuwa inanufaika katika kituo hicho. Hichi nilikuwa naomba kuelezea katika ukurasa wa 23 ya vipaumbele vya Taifa.

Mhe. Naibu Spika, nikija katika suala la uingiaji wa wageni katika hotuba imeonesha kama kutoka Julai mpaka Disemba idadi ya wageni ilishuka na tukapata idadi ya wageni 102,746 ukilinganisha na mwaka 2019 ambapo ilikuwa dunia haijaathirika na *Corona* ambapo tulipata wageni 335,374.

Kwa hiyo, hali ya wageni kuanzia mwezi wa Novemba, Disemba na Januari imekuwa ni kubwa. Lakini kama wachangiaji ambao wengi ambao wamechangia naomba nikiri kwamba ni kweli kuwa soko tunalo na baada ya *Corona* limebadilika soko letu lilikuwa Ulaya ya Magharibi ambapo tulikuwa na wageni ambao tunasema kipato chao na mazingira yao ni mazuri. Lakini kutokana na hali ya *Corona* soko limebadilika tumekuwa na soko la Ulaya Mashariki ambapo kipato chao na hali yao ni tofauti na sio hali ile ambayo ni kwamba tumeizoea.

Lakini ambazo ni changamoto zipo lazima tukubaliane nazo ni kutokana na hali ya maradhi duniani ambayo ipo na sekta yetu. Kama serikali tunategemea utalii wa ndani ni sawa lakini asilimia kubwa Zanzibar tunategemea utalii kutoka nje. Soko letu la asili limeathirika kwa kiwango kikubwa. Kwa hiyo, kama serikali tumeruhusu soko jengine lakini hizi changamoto ambazo zipo lazima tukubaliane nazo na tukubaliane nazo kama serikali tumejipanga kukabiliana nazo ingawaje kipato chao lazima tukiri ni kidogo na si kama kile ambacho tumekizoea.

Kwa hiyo, hili halikuja kama serikali tumeamua lakini limekuja baada ya kutokana na hali ya dunia na maradhi ambapo nchi nyingi zimefunga mipaka yake na raia wake wamekuwa hawaruhusiwi kutoka na kuja katika Sekta ya Utalii. Kwa hivyo, hili naomba lieleweke hivyo ni mabadiliko ya upepo lakini kama serikali tumejipanga kuhakikisha hali ya *Corona* ikirudi katika hali yake ya kawaida soko letu mama mpaka sasa wale mawakala ambao tunaendelea kuwasiliana nao ili hali ikitulia lile soko letu litarudi na hili ambalo tunalo tunaendelea kuli-*maintain* hii ndio mipango ya serikali na naomba ieleweke hivyo.

Pamoja na changamoto ya soko jipya tunajipanga nalo kuhakikisha kuwa tunapunguza baadhi ya changamoto zikiwemo suala la maadili ambalo wachangiaji wengi wamechangia kuwa watalii ambao wapo wanatembea wakiwa karibu uchi kabisa na nguo ambazo hazistahiki. Lakini hili kama wizara tumelisimamia na tumeshatoa mwelekeo kwa sababu sheria zipo lakini ni *enforcement* ya sheria. Kwa hiyo, tunachotumia sasa hivi ni kuwasiliana na vyombo vya ulinzi ni kuhakikisha tunawasimamia wanaondoa misafara ya watalii, wenye mahoteli sote kwa pamoja kuhakikisha kuwa tunasimamia kuwaeleza ile miiko na maadili ya Zanzibar, ili wanapokuja hapa wafuate kwa vile ambavyo inahitajika na sio kama hali ambayo iko sasa. Kwa hiyo, hili tumelijua kama serikali na tunalifanyia kazi tukishirikiana na taasisi binafsi.

Naomba ieleweke utalii mkubwa asilimia thamanini na tisini tunafanya kazi na Sekta Binafsi wakiwemo *ZAT*, *ZATO* pamoja na *ZatGo* na ndio wadau ambao kwa asilimia kubwa wapo katika kutafuta *connection* ya kuleta wageni hapa nchini kwetu wakishirikiana na serikali, kwa hiyo hili tunalifanyia kazi.

Lakini pia Mhe. Naibu Spika, katika mwelekeo huu naomba nichangie katika punguzo la ushuru. Mwelekeo unaeleza katika jitihada zilizochukuliwa kuhakikisha kama hali ya uchumi

inakuwa nzuri serikali imetoa punguzo la kiwango cha kutozea ushuru wa hoteli kutoka asilimia 18 hadi 12.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na punguzo hili ambalo serikali imetoa naomba nikiri bado kuna changamoto kubwa ya wenye mahoteli na wenye huduma zote za kitalii kulipia leseni zao kulipia kodi ambazo zinastahiki kutokana na athari ya *Corona*. Mara nyingi kumekuwa na malalamiko lakini kama wizara na serikali tumekuwa tukihakikisha kuwalazimisha kuwalipia angalau sio kama ni punguzo lakini wanachotaka ni kusamehewa, kwa kweli hiyo inakuwa ni ngumu kama hoteli mwaka mzima usamehewe kodi moja kwa moja hilo haliwezekani. Lakini kama ni serikali katika kuona changamoto ambazo zimepatikana kutokana na ugonjwa wa *Corona* tumepunguza huu ushuru ili angalau na wao wapate chochote katika kuhakikisha wanaendesha huduma zao za kitalii kama ambavyo inastahiki.

Mhe. Naibu Spika, nikija katika suala la Utalii wa Ndani wachangiaji wengi nao wamechangia sana Utalii wa Ndani na Utalii kwa Wote. Kama wizara tumejipanga kuhakikisha kuwa dhana ya Utalii wa Ndani tunaendelea kutoa taaluma kwa wanachi wetu kuhakikisha kuwa wanajua umuhimu wa vivutio na kuvilinda na kuweka katika mazingira safi. Katika hili dhana ya Utalii wa Ndani ndio maana tumeanzisha Kampeni ya Usafi ili kuhakikisha tunahamasisha watu wakati wa Kampeni ya Usafi, lakini pia tunatoa elimu na taaluma kwa wananchi mbali mbali juu ya umuhimu wao wa kushiriki katika shughuli za kiutalii pamoja na kuwa salama kwa watalii wetu wanapokuwepo nchini. Ukizingatia pia kumekuwa na taarifa ya hali ya usalama wa watalii kutoka maeneo mbali mbali, kumekuwa na taarifa pengine ya kuporwa na vitu kama hivyo. Kwa hiyo, kubwa tunaloendelea ni kutoa taaluma lakini pia na kuchukua hatua stahiki kwa wale ambao wanafanya vitendo hivi ambavyo vinahatarisha amani kwa wageni wetu.

Mhe. Naibu Spika, wachangiaji wengi pia walichangia suala la Mambo ya Kale pamoja na umuhimu wa kutumia vituo vyetu vya kihistoria katika kuhakikisha tunatunza utalii wetu. Mimi nakubaliana na wao asilimia mia na ni katika vipaumbele tumeweka katika wizara kuhakikisha hata vivuto vipya ambavyo tunaibua vingi vyao vipo katika maeneo ya kihistoria na ukitizama kwa upande wa Unguja tunayo Mvuleni ambayo inaelezea ni maeneo ya Wareno ambapo walikuwepo tunayo Fukuchani, tunayo Mkamandume kwa upande wa Pemba. Lakini pia tuna maeneo kwa mfano kama Mkumbuu ambayo tumeyalenga kama itakuwa ni vivutio ambavyo vitaboreshwa ndani ya miaka hii mitano na yote ni maeneo ya kihistoria ambapo mtalii atakapokuja atapata historia ya Zanzibar.

Lakini Mhe. Naibu Spika, kwa nafasi ya kipekee maeneo ya Mji Mkongwe tumepanga kuuboresha zaidi pamoja na changamoto ya kuwa tuna uchakavu wa majengo lakini serikali tumepanga kufanya kazi na taasisi binafsi ili waweze kuwekeza katika majengo yale na kuyaboresha na kuupa hadhi Mji Mkongwe, ili utuingizie pesa zaidi kulikoni unavyoingiza pesa sasa hivi. Ukitizama Mji Mkongwe wote ni sehemu ambayo ya historia na ni sehemu nzuri.

Kwa hiyo, hatua mbali mbali kama serikali tumekuwa tukipanga ikiwemo kufanya kazi na hizo sekta binafsi ili waweze kuwekeza katika maeneo yetu ya kihistoria hata katika maeneo yetu ambayo sasa hivi tunayatumia kama Makumbusho milango iko wazi. Tunavyofanya kama serikali ni kupanga utaratibu wa jinsi gani tutafanya kazi na sekta binafsi, ili kuhakikisha serikali inapata, lakini na wawekezaji wanapata na huduma nzuri ambazo zinaendana na wakati wa karne hii ya 21 kwa wageni wetu zinakuwa zinapatikana katika maeneo yetu ya kihistoria.

Mhe. Naibu Spika, pia kulikuwa na hoja ambayo ilichangiwa sana kuhusiana na hadhi ya utalii tuwe na *focus* ya kuwa na utalii wa hali ya juu na hii tumeipanga kwa ajili ya Kisiwa cha Pemba. Tulisema kama serikali Pemba tunataka kufungua kiwe kituo cha uwekezaji. Lakini katika Sekta ya Utalii tunataka kuwekeza watalii ambao tunasema kuwa *high tourism*, ule utalii ambao ni wa daraja la juu, wanaokwenda Pemba hoteli zote ambazo zitajengwa Pemba katika awamu hii tume-*focus* hoteli za hadhi ya juu kuanzia nyota tano na ambazo wageni watakaokwenda kule watakuwa ni wale *high spend* ambao wana pesa wanakwenda ku-*spend*. Itakuwa ni utalii katika maeneo maalum ili kupunguza hii changamoto ya utalii ambao ni rahisi wa bei nafuu ambao upo umeenea katika maeneo yetu.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache, naunga mkono hoja. Nakushukuru sana na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante Mhe. Waziri. Mchangiaji anayefuata sasa hivi ni Mhe. Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, baada ya hapo atafuata Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed ambaye ni Waziri Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi.

**Mhe. Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa ruhusa yako nichukue fursa hii kuungana na wajumbe wengine kwanza kuanza kumshukuru Mwenyezi Mungu.

Vile vile kuchukua fursa hii kutoa pole kwa taifa letu la Zanzibar kwa msiba ambao umetokea. Pia na mimi nichukue fursa hii kushukuru na kuwapongeza Wizara ya Nchi (OR) Fedha na Mipango kwa kutuandalia kitabu kizuri ambacho kinafahamika.

Mhe. Naibu Spika, mimi nitakuwa na machache ya kuelezea ikiwa ni mchango wangu katika hotuba hii. Kipekee kabisa niwapongeze sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa michango yao mizuri sana, lakini vile vile kwa michango yao ambayo inalenga kujenga na pia inalenga kuisaidia serikali kufanya vizuri katika mwaka huu tulionao wa 2021 hadi 2024 na kuendelea.

Mhe. Naibu Spika, kipekee kabisa niwapongeze wajumbe wote waliochangia hotuba hii. Mimi niseme karibu asilimia 90 ya wajumbe ambao wamechangia hotuba hii, hakuna mjumbe hata mmoja aliyechangia bila kugusa suala zima la programu ya ajira kwa vijana. Mhe. Naibu Spika, hii inaonesha wazi wazi kwamba taifa letu la Zanzibar linakabiliwa na changamoto kubwa ya ajira kwa vijana, pia wajumbe wameweza kuonesha kwamba asilimia kubwa ya watu wanaoishi Zanzibar ni vijana, kwa hivyo wameguswa na hilo na mimi nawashukuru sana kwa michango yao mingi ya kujenga.

Mhe. Naibu Spika, nichukue fursa hii kutoa ahadi kwamba nitashirikiana na Waheshimiwa Wajumbe wote, ili kuhakikisha tunafanya marekebisho makubwa kwenye suala hili la programu ya ajira kwa vijana. Vile vile tutahakikisha tunasimamia vyema yale malengo ambayo serikali imejiwekea, nayo sio mengine bali ni kuwaendeleza vijana kujikwamua kiuchumi yanafikiwa kwa asilimia 100.

Mhe. Naibu Spika, ukiangalia katika ukurasa wa 23 kwenye vipaumbele vya kitaifa kwa mwaka 2021/2022, kipaumbele namba 7 kimezungumza moja kwa moja kuendelea na utekelezaji wa programu ya ajira kwa vijana. Kwa hivyo, naipongeza sana Wizara ya Fedha kwa kuliona hili na naishukuru.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na michango ya wajumbe ambayo imetolewa, mimi nilikuwa nataka nitowe ufafanuzi ufuatao.

Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba nikiri kwamba miradi mingi iliyolengwa kwa ajili ya vijana haikuweza kufanyakazi, haikuweza ku-*deliver* matokeo hayakutoka kama ilivyotarajiwa. Lakini Mhe. Naibu Spika, Wizara yetu ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa mwaka huu wa 2021/2022 tumejipanga vizuri ili kuhakikisha tunaisimamia miradi hii. Vile vile tumejipanga kama wizara, kubuni miradi mikubwa zaidi ambayo itawawezesha vijana waweze kufanya kazi hizi na kujiajiri wenyewe, lakini inapobidi pia waweze kuajiriwa.

Mhe. Naibu Spika, pia niseme kwamba wizara yetu imejipanga kutengeneza miradi ambayo sio tu itategemea bajeti kuu ya serikali kwa maana ya bilioni tatu, bali tutafanya miradi ambayo tunaweza kutafuta wadau mbali mbali wa ndani na nje ya nchi, waweze kutusaidia ili kuweza kuwa-*support* vijana katika kazi zao mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, naomba nikubaliane na Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Mkwajuni, alisema kwamba programu zetu zote tulizokuja nazo zote ni nzuri, lakini bila ya usimamizi thabiti haiwezi kutekelezeka. *(Makofi)*

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, na mimi nachukua ahadi hiyo kwamba tutajitahidi sana kusimamia miradi hii, kwa sababu kuna miradi ime-*fail* kwa sababu tu usimamizi haukuwepo sawa sawa.

Mhe. Naibu Spika, nataka nitowe rai moja. Hii rai naomba sana tusaidiane na Waheshimiwa Wawakilishi waliomo humu. Wawakilishi wa Majimbo ambao wao ni wadau wakuu wa vijana wetu, lakini hata Wawakilishi wa Viti Maalum kama kinamama, kama watu wenye ushawishi mkubwa na wawakilishi wengi wamechangia wameonesha kabisa nguvu ya kinamama na nguvu ya mwanamke katika kuleta maendeleo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba kuna changamoto ya vijana wetu baadhi ya vijana wanakuwa wanachagua kazi za kufanya. Serikali inaweza ikapanga mipango mizuri na thabiti kwa ajili yao, ikatoa gharama kubwa kwa ajili yao na ikaanzisha ile miradi kwa ajili yao. Lakini vijana wale mwisho wa siku wanaondoka, mwisho wa siku hawatoi mashirikiano na mwisho wa siku wanataka kazi zile za kukaa maofisini, wakati pengine vijana wale wengi wao elimu yao haiwezi kukidhi kuwepo maofisini.

Kwa hivyo, nitowe rai hii kwa kushirikiana na Waheshimiwa Wawakilishi wa Majimbo pamoja na Viti Maalum, tuhakikishe pia na sisi tunatoa elimu na tunakaa na vijana wetu ili kuweza kuwaelewesha juu ya mipango yetu mizuri ya serikali, vile vile kuhakikisha na wao wanakuwa na moyo wa kizalendo wa kujenga taifa lao na pia kuwapa faida za serikali pale itakapojikita kwa ajili yao, basi na wao wawe tayari kuhakikisha tunashirikiana kwa pamoja, ili kuweza kufanya vizuri.

Mhe. Naibu Spika, mimi niseme hata ilani yetu ya uchaguzi ya mwaka 2025 imezungumza sana suala la ajira na imezungumza sana kwa upande wa vijana, kwa sababu vijana ndio ambao wanaonekanakabisa wanatakiwa kupata *opportunity* kutokana na umri wao.

Mhe. Naibu Spika, lakini zile ajira hazitoweza kufikiwa endapo vijana wale watakuwa pia na wao kwa upande wao hawako tayari. Ninachomaanisha Mhe. Naibu Spika, suala la

kuwawezesha vijana kiuchumi lina pande pili, lina pande ya serikali ambayo inatoa mkono wake na msaada wake, lakini lina pande ya pili ya vijana ambao ndio walengwa.

Kwa hivyo, niwaombe sana na nitowe wito, wizara kama wizara tumejipanga vizuri tutapita kijiji kwa kijiji, mtaa kwa mtaa kuhakikisha tunawapa elimu vijana wetu, ili waweze kuona faida na tija ya programu zile. Vile vile niseme kwamba wizara yetu itajitahidi sana kuhakikisha inajirekebisha kwenye jambo moja la ushirikishwaji wa vijana kabla ya kufanya mipango endelevu. Ushirikishwaji huu tutaufanya tutakapokuwa na wataalamu wetu. *(Makofi)*

Kwa mfano, tutajitahidi sana kuhakikisha tunawapa vijana nyenzo ambazo zinaendana na mazingira halisi waliyokuwanayo, nyenzo ambazo zinaendana na mazingira halisi ya uwezo wao vijana waliokuwanayo.

Kwa mfano, tutajitahidi kwa vijana ambao wamebobea kwenye mambo ya uvuvi kuwatengenezea mazingira ya kuwanunulia zile boti kwa ajili ya uvuvi, sio boti kwa ajili ya kutembelea na mambo mengine hatimaye zikakosesha faida na kuingiza pato katika serikali.

Vile vile niseme Mhe. Naibu Spika, wizara yetu pia imejipanga kuhakikisha vijana hawa programu hii itakapotekelezwa, basi tutahakikisha vijana hawa wanafanya programu hii na baadae wao wanapata kipato kwa ajili ya kujiendeleza na vile vile vijana watakaokuja waweze kupata ile faida ambayo itakuwepo pale, ili waweze kuendeleza programu hii.

Mimi ninachokisisitiza Mhe. Naibu Spika, ni kuhakikisha kwamba mipango ya serikali ambayo imewekwa inawasaidia sana vijana na tutajitahidi kama wizara. Wito wangu na ombi langu kwa Waheshimiwa Wajumbe tushirikiane kwa pamoja, hili sio suala sio la wizara pekee bali ni suala la jamii nzima na wawakilishi wetu ni miongoni mwa viongoni na ni miongoni mwa wazazi na walezi katika jamii.

Mhe. Naibu Spika, niseme jambo jengine suala zima la michezo. Halikuzungumzwa moja kwa moja kwenye mpango huu, lakini mimi niseme katika hii hii programu ya ajira kwa vijana, wizara imejipanga vizuri, ili kuhakikisha programu hii ya michezo tunaigeuza kutoka kwenye starehe kuja kwenye suala la kiajira au kibiashara. Imeonekana moja kwa moja Mhe. Naibu Spika, michezo inaleta tija, inaleta ajira na inaleta *opportunity* mbali mbali, ikiwemo kuitangaza nchi yetu katika mataifa mengine. Kwa hivyo, wizara italisimamia vyema na nina amini pia Wizara ya Fedha na Mipango katika programu ya ajira kwa vijana watatuongezea fungu kubwa ili tuweze pia kuingiza michezo na kui-*promote* kuweza kufanya vizuri katika nchi yetu.*(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa na mimi niungane na wajumbe wengine kuwapongeza sana watendaji pamoja na Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, kwa kuandaa kitabu kizuri, kwa kuandaa mwelekeo mzuri na mimi nasema naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante sana Mhe. Waziri, nakushukuru sana. Sasa nimpe nafasi Mhe. Dkt. Khalis Salum Mohamed Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Mhe. Waziri, karibu sana.

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Naibu Spika, naomba na mimi nichukuwe fursa hii kuchangia hoja ya Mhe. Waziri, kuhusu Hotuba ya Mwelekeo wa Hali ya Uchumi Mpango wa Maendeleo na Bajeti kwa mwaka 2021/2022 hadi 2023/2024.

Mhe. Naibu Spika, niungane na Waheshimiwa Wajumbe kutoa pole kwa Mhe. Rais Dkt. Hussein Ali Mwinyi, lakini pia kutoa pole kwa wana familia na wanachama wote wa *ACT*, lakini na kwa Wazanzibari na Watanzania wote kwa kuondokewa na kiongozi wetu mkuu Maalim Seif Sharif Hamad Mwenyezi Mungu amlaze mahala pema peponi Amina.

Pia nichukuwe fursa hii kumpa pole Mhe. Rais John Pombe Joseph Magufuli kwa kuondokewa na Katibu Kiongozi ndugu John Willium Kijazi, nawapa pole pia wanafamilia ndugu na marafiki wa marehemu Kijazi.

Pili, Mhe. Naibu Spika, nitowe pongezi za dhati kabisa kwa Serikali yetu ya Awamu ya Nane inayoongozwa na Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi, kwa mwanzo mzuri sana wa kutekeleza ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, lakini pia kutekeleza mipango ya serikali kwa kasi kubwa sana. *(Makofi)*

Vile vile niipongeze Awamu ya Saba iliyoongozwa na Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kazi nzuri sana ya utekelezaji wa bajeti katika kipindi cha kwanza bajeti ya mwaka 2020/2021.

Pia nichukuwe fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha na Mipango lakini na timu yake yote, watendaji wakiongozwa na Katibu Mkuu kwa hotuba nzuri sana iliyoandaliwa. Mapitio yameelezwa vizuri lakini na mwelekeo kwa miaka mitatu umefafanuliwa vizuri sana hongereni sana kwa taarifa hii. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, ukurasa wa 2 na wa 3 wa kitabu hiki umezungumza mafanikio, lakini mafanikio haya yamezungumzwa kwa ufasaha mkubwa na uwazi, kwamba yamesababishwa na baadhi ya mambo ambayo yamechukuliwa na serikali yetu, Serikali ya Awamu ya Saba, lakini pia yanaendelezwa na Serikali ya Awamu ya Nane.

Mhe. Naibu Spika, naomba niyataje. Pamoja na changamoto zilizoikumba dunia ya kuwepo ugonjwa huu wa *Covid 19*, lakini maamuzi ya serikali kwanza ya kutoweka *lockdown* yamesaidia sana kuimarisha uchumi wetu na kufikia hapa ulipo. Pia kuruhusu safari baina ya Zanzibar na Tanzania Bara imesaidia sana kuchangia katika maendeleo ya kiuchumi na ya kijamii tuliyonayo hivi sasa. Vile vile kufungua safari za ndege kutoka nje na kuruhusu watalii kuingia katika nchi yetu, ni miongoni mwa mambo ambayo yamesaidia sana.

Mhe. Naibu Spika, niseme pamoja na changamoto tuliyonayo katika dunia hii ya *Covid*, lakini kwa mtizamo wangu Mhe. Naibu Spika, ni kwamba tatizo hili lipo kidunia na kwa wenzetu kama ilivyosemwa hapa limewakumba zaidi kuliko sisi, alizungumza Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali. Lakini matatizo haya yanapotokea katika dunia, inabidi na sisi tujifunze kuishi nayo kwa tahadhari, hatuwezi kuyakimbia, hatuwezi kujifungia ni kutafuta namna ya kupambana nayo ili maisha yaendelee. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa hili naipongeza sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inayoongozwana Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, lakini na Serikali yetu ya Mapinduzi inayoongozwa na Mhe. Hussein Ali Hassan Mwinyi kwa misimamo yao, kwa sababu bila ya hivyo kunaweza kukahatarisha maisha zaidi kuliko hata mahatarisho ya maisha yanayotokana

na ugonjwa huo. Kwa hivyo, mimi napongeza sana na nashukuru sana kwa juhudi hizo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, lakini niipongeze sana serikali kwa kupunguza kodi na kurahisisha shughuli za biashara. Kitabu kinatueleza kwamba kodi imepungua ya ongezeko la thamani kutoka asilimia 18 hadi asilimia 15, lakini hii pia inatoa unafuu mkubwa sana kwa wafanyabiashara wetu, lakini inatoa unafuu kwa wawekezaji wetu, lakini kuna kodi ya vifaa vya uvuvi navyo vimepunguzwa, kuna kodi ya ushuru wa hoteli imepungua kutoka asilimia 18 hadi asilimia 12, lakini pia wafanyabiashara wadogo wadogo nao wamepunguziwa kodi ya kutokulipa shilingi 1,000 hadi shilingi 2,000 kwa siku na sasa wanatakiwa walipe mara moja shilingi 30,000 kwa mwaka. Yote hii imewekwa maalum kwa kusaidia kuchochea biashara, kuchochea uwekezaji, lakini pia kuongeza kipato kwa wananchi na bila shaka kipato kikiongezeka mwisho wa habari na kodi za serikali zitaongezeka, kwa sababu watu wengi sana watashiriki katika biashara na uwekezaji ikiwa kodi zimepungua.

Mhe. Naibu Spika, kwenye mapitio ya mpango wa maendeleo iko kwenye ukurasa wa 5 na ukurasa wa 6. Niipongeze sana serikali yetu kwa mafanikio makubwa na imeelezwa kwamba asilimia ya watu wetu wanaoishi katika umaskini uliokithiri, ilipangwa ikifika mwaka 2019/2020 basi kiwango hicho kiwe ni cha asilimia, lengo lilikuwa ni asilimia 10, lakini lengo lililofikiwa ni asilimia. Samahani, lengo lililofikiwa ni asilimia 10 lakini mpango ulikuwa tufikie asilimia 9 nukta. Samahani tena.

Mhe. Naibu Spika, lengo lilikuwa ni asilimia 10, lakini sisi tumeshusha mpaka kufikia asilimia 9.3. Pia tumeweza kufikia uchumi wa nchi zenye uchumi wa kati *low middle income* ni mafanikio makubwa sana, lakini pia tumeweza kufikia matarajio ya kuishi *life expectant* ya miaka 65, kutoka ile ya miaka 48 miaka 30,000 iliyopita.

Tumeweza pia kupunguza mfumko wa bei, kwa maana ya kuudhibiti kuwa chini ya tarakimu moja na kwa mwaka 2019 mfumko wa bei ulikuwa ni wa asilimia 2.7. Haya ni mafanikio makubwa sana pamoja na changamoto zilizoikumba dunia, lakini sisi tumeweza kufikia mafanikio haya, kwa hivyo ni lazima sana tujivunie. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, katika ukurasa wa 12 *item* ya 7.3, imezungumzia suala la deni la taifa. Hapa nipongeze tena kwa sababu pamoja na kwamba uwiano wa deni la taifa kwa uchumi limeongezeka kidogo, lakini bado liko chini ya kile kiwango kinachokubalika kimataifa. Ni asilimia 22 na inaonesha bado uweze wetu wa kukopa na fursa ya kukopa ikipatikana upo, kwa sababu deni hili ni himilivu. Ziko nchi sitaki kuzitaja hapa, lakini uwiano wa deni na *GDP* yao kwa maana uchumi wao ni karibu asilimia 43 nazijua ni mkubwa mno karibu watafikia kiwango cha mwisho cha asilimia 50. Sisi tuko asilimia 22 na hapa mimi nasema kwamba Mhe. Naibu Spika, tusiogope kiwango hiki bado deni ni himilivu asilimia 22 lakini tuwe tunakopa kwenye miradi yenye tija na itakayoweza kuchochea uchumi wetu, hilo ndio jambo la msingi. Tukope kwa miradi ambayo itachochea ukuaji wa uchumi lakini itakuwa na tija. Hakuna nchi isiyokopa katika dunia na sisi kwa vile uchumi unaendelea ni muhimu kukopa lakini tukope pale panapo haja ya kukopa kwa miradi itakayokuwa na tija katika uchumi wetu.

Mhe. Naibu Spika, ukurasa wa 18 hadi 20 umeelezea mwelekeo wa hali ya uchumi kwa mwaka 2021/22 hadi 2023/2024. Mwelekeo umewekwa vizuri wa kuhakikisha kwamba tunazingatia zile sekta ambazo ziliathirika zaidi na hili janga la *COVID 19* na sekta hizi ni pamoja na Sekta ya Utalii, Sekta ya Shughuli za Biashara, lakini pia uwekezaji katika uchumi

wa buluu, viwanda vidogo vidogo, bila ya kusahau huduma za kijamii kwa maana elimu, afya na upatikanaji wa maji safi na salama. Kwenye hili nashukuru na napongeza sana kwamba mwelekeo huu umezingatia Dira ya Maendeleo ya 2050. Lakini pia imezingatia Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2020/2025. Lakini pia mikakati yetu ya kukuza uchumi na nashukuru kwamba sasa hii itakuwa ni bajeti ya mwanzo ya utekelezaji wa hii Dira ya 2050.

Mhe. Naibu Spika, nampongeza sana Mhe. Waziri lakini naipongeza pia timu yake nzima kwa kuweka vipaumbele vizuri sana kwa miaka mitatu ijayo, lakini hata ukivitizama na vile vipaumbele vilivyowekwa kwa mwaka 2021/2022 ni vipaumbele ambavyo vimewekwa kimakini sana. Mhe. Mjumbe mmoja alizungumzia suala la umwagiliaji maji nimeliona lipo, ukiangalia na vipaumbele vyengine vyote suala la umwagiliaji maji ni muhimu sana na kwa ujumla uzalishaji wa ndani katika kipindi hiki ni muhimu sana iwe ni Sekta ya Kilimo, Sekta ya Uvuvi, Viwanda Vidogo Vidogo na nasema kwa sababu ya hali ya dunia ilivyo.

Masuala ya kilimo ni muhimu kwa sababu ya uhakika wa chakula *(food security)*, uvuvi pia mbali ya kwamba tutajenga uwezo wetu wa kusafirisha na kupata fedha za kigeni, lakini pia itatusaidia katika kukuza uhakika wa chakula, upatikanaji wa chakula katika nchi na kutokana na changamoto hii iliyoingia ya ugonjwa huu katika dunia ni kwamba sisi tuweze kujitoleza ndani. Sasa vipaumbele hivi navipongeza sana na ningeomba wenzetu wa Sekta Binafsi *(Private Sector)* wa ndani wahamasike katika kushiriki kuwekeza katika vipaumbele vilivyowekwa na serikali. Yapo maeneo ambayo serikali itaingia moja kwa moja, lakini yapo maeneo Sekta Binafsi ya ndani na nje ishiriki katika utekelezaji wa vipaumbele hivi, lakini pia utekelezaji wa vipaumbele hivi, lakini pia utekelezaji wa miradi mikubwa.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ambalo ningependa kulichangia ambalo lilichangiwa pia na baadhi ya Wajumbe ni ukusaji wa mapato, tuna vipaumbele vya mwaka 2021/2022 lakini vipaumbele hivi vinahitaji fedha, tuna bajeti ambayo imepangwa ya trilioni 1.5 lakini mapato ya ndani kutokana na vyanzo vya ndani ni karibu trilioni 1.105, ni karibu asilimia 74.4. Mhe. Saada Mkuya Salum alizungumzia hapa kwamba baadhi ya fedha tunazozitarajia kutoka nje kutokana na hali hii zinaweza zisiwe *realize* zisipatikane. Lakini chanzo cha uhakika ni vyanzo vya mapato vya ndani, sasa mimi naomba kwamba hapa tushirikiane si suala la serikali peke yake, si suala la wizara inayohusika na Fedha na Mipango, si suala la taasisi za ukusanyaji wa mapato peke yake, lakini sote tunahusika katika kuimarisha vyanzo vya mapato. *(Makofi)*

Wajumbe wa Baraza tuhamasishe wananchi wetu na tuwahamasishe kwamba pale wanaponunua huduma na bidhaa wadai risiti hilo ni jukumu ambalo sisi tunaliweza, lakini na wananchi washajihike kuhakikisha kwamba wanaponunua bidhaa, wanaponunua huduma wanapata risiti. Kwa namna hiyo, watakuwa wanachangia katika ukusanyaji wa mapato. Lakini na wenzetu vyombo vinavyohusika ukusanyaji wa mapato ni muhimu sana kuhakikisha kwamba wale wote wanaostahiki katika kulipa kodi za serikali basi wanasajiliwa ni jambo muhimu sana. Nadhani kulikuwa na utaratibu Mhe. Waziri atakuwa anaujua wa *block registration* nadhani huo uangaliwe vizuri, ufanyiwe kazi vizuri ili wote wanaostahiki kulipa kodi za serikali wanazilipa.

Lakini kukusanya ni jambo moja udhibiti wa upotevu wa mapato ni jambo jengine na hili sote tuna nafasi ya kushiriki katika kuhakikisha kwamba mapato ya serikali hayavuji lakini pia yanatumika kwa shughuli zinazostahiki. Sasa hili si jambo la wizara moja ni jambo letu sote nawaomba wananchi, nawaomba wafanyabiashara hasa wale wenye tabia ya kufanya *wrong declaration* wapo wachache ambao hawa-*declare* bidhaa zao kama zilivyo

wanaofanya *under declaration* waache kufanya hivyo kwa sababu wakifanya hivyo wanaharibu uchumi wa nchi hii.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo nirudi kumpongeza Mhe. Rais, nimpongeze waziri, niwapongeze watendaji wote mwelekeo ni mzuri na naamini sasa ni wajibu wetu sote kutoa ushirikiano wa kutosha kwa haya yaliyoletwa kwenye mwelekeo na itakapokuja bajeti basi tusimamie kwenye kuyatekeleza. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante sana Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Mchangiaji anayefuata ni Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha na Mipango. Karibu.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha na Mipango:** Mhe. Naibu Spika, awali ya yote kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii, baada ya kusema hayo nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutuwezesha leo kuamka salama wa afya na amani. Lakini nipende kuchukua nafasi hii ya kipekee kabisa kumpa pole Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi kwa kuondokewa na aliyekuwa Makamu wetu wa Kwanza wa Rais, Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad kusema la kweli alikuwa ni mwanasiasa mahiri, kiongozi mchapa kazi ambaye aliipenda sana nchi yake.

Pia nichukue nafasi hii niwape pole ndugu, familia na jamaa wa marehemu lakini bila kusahau wanachama wa Chama cha *ACT* Wazalendo kwa sababu alikuwa ndio Mwenyekiti wao wa Chama Taifa, na Wazanzibari wote kwa ujumla. *(Makofi)*

Lakini nitumie nafasi hii vile vile kumpa pole Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuondokewa na Katibu Mkuu wetu Kiongozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Marehemu Balozi John Kijazi na yeye alikuwa ni mtendaji mahiri ambaye karibu umri wake wote wa maisha yake alitumikia katika kuihudumia Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Baada ya pole hizo, Mhe. Naibu Spika, tarehe 16/12 niliwasilisha Mwelekeo wa Hali ya Uchumi, Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 hadi 2023/2024 ambayo haya ndio kwa mujibu wa matakwa ya Katiba ya Zanzibar ibara ya 105 inaelekeza hivyo. Lakini vile vile Sheria ya Fedha za Umma Nam. 12 ya Mwaka 2016 *section 39 sub section 1* inaeleza hivyo pamoja na Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi pia zinaelekeza hivyo. Kwa mujibu wa matakwa ya kisheria ilinibidi niwasilishe Mwelekeo huo wa Hali ya Uchumi, Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Serikali kama ambavyo nimenukuu miongozo yote hiyo ya kisheria ikinitaka.

Mhe. Naibu Spika, lengo kubwa ilikuwa ni kuwapa fursa Waheshimiwa Wawakilishi kuchangia kutoa mawazo yao, ili sasa wizara ambayo inashughulika na masuala ya fedha na mipango yaani Wizara yetu chini ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango tuchukue mawazo yao na kwenda kuandaa sasa mpango wa serikali na bajeti ya serikali ambapo tutawasilisha katika kikao kinachofuata.

Baada ya kusema hayo nishukuru sana Waheshimiwa Wawakilishi ambao walibahatika kuchangia na kusema la ukweli michango yao yote tumeichukua na *in shaa Allah* tutakwenda kuifanyia kazi pale ambapo tutakapoandaa mpango huu.

Lakini nitumie nafasi hii vile vile kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri ambao waliweza kuchangia mpango ambao jumla yao walikuwa Mawaziri watano, pia waliweza kutoa

ufafanuzi kwa baadhi ya hoja mbali mbali ambazo Waheshimiwa Wawakilishi walipenda au waliona kuna haja ya kuelezewa na kufafanuliwa kwa kina. Mhe. Naibu Spika, naomba niwatambue.

1. Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali.
2. Mhe. Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo.
3. Mhe. Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale
4. Mhe. Waziri wa Habari, Vijana,Utamaduni na Michezo
5. Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi.

Hawa ndio baadhi ya Mawaziri ambao waliweza kuchangia, lakini vile vile Mwelekeo huu wa Mpango na Bajeti uliweza kuchangiwa na jumla ya Wawakilishi 42 ambao sita kati yao walichangia kwa njia ya maandishi na 37 walichangia kupitia kuwasilisha au kuzungumza ndani ya Baraza lako. Nao vile vile Mhe. Naibu Spika, naomba niwatambue kwa wale waliochangia kimaandishi ni:-

1. Mhe. Kombo Mwinyi Shehe
2. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf
3. Mhe. Mohamed Mgaza Jecha
4. Mhe. Miraji Khamis Mussa
5. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa
6. Mhe. Mgeni Hassan Juma (wewe Mhe. Naibu Spika)

Kwa wale ambao walichangia kwa kuzungumza naomba pia na wao niwatambue:-

1. Mhe. Habib Ali Mohamed
2. Mhe. Bakar Hamad Bakar
3. Mhe. Shamata Shaame Khamis
4. Mhe. Suleiman Makame Ali
5. Mhe. Shaib Hassan Kaduara
6. Mhe. Omar Said Shaaban
7. Mhe. Juma Makungu Juma
8. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman
9. Mhe. Maryam Thani Juma
10. Mhe. Shaaban Ali Othman
11. Mhe. Bihindi Hamad Khamis
12. Mhe. Panya Ali Abdalla
13. Mhe. Hassan Khamis Hafidh
14. Mhe. Hassan Hamad Omar
15. Mhe. Juma Ali Khatib
16. Mhe. Issa Haji Ussi
17. Mhe. Hamza Hassan Juma
18. Mhe. Asha Abdalla Mussa
19. Mhe. Suleiman Haroub Suleiman
20. Mhe. Said Saleh Salim
21. Mhe. Fatma Ramadhan Mohamed
22. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf
23. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma
24. Mhe. Ameir Abdalla Ameir

25. Mhe. Haji Shaaban Waziri
26. Mhe. Ali Suleiman Ameir
27. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma
28. Mhe. Harusi Said Suleiman
29. Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis
30. Mhe. Rukia Omar Ramadhan
31. Mhe. Yahya Rashid Abdulla
32. Mhe. Sulubu Kidongo Amour
33. Mhe. Zawadi Amour Nassor
34. Mhe. Ali Abdulgulam Hussein
35. Mhe. Kombo Mwinyi Shehe
36. Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum
37. Mhe. Sabiha Filfil Thani

Hawa ndio wale waliochangia kwa kuzungumza humu Barazani.

Mhe. Naibu Spika, sasa Waheshimiwa Wajumbe walieleza vitu vingi ambavyo vyengine tumevichukua, vyengine tutavifanyia kazi na mengine mengi tutawasilisha kwa maandishi. Lakini kutokana na muda kuna mambo ya muhimu ya msingi haya nitayawasilisha kwa kuchangia na mimi au ku-*wind up* hotuba yangu kwa leo.

Waheshimiwa Wawakilishi wengi walizungumzia suala la miradi, kweli tumeweka miradi mingi lakini tumeweka kwa sababu gani. Hatukuweka kwa ajili ya kuongeza kurasa za kitabu, tuliweka kwa sababu ya malengo mahsusi. Waheshimiwa Wawakilishi mtakumbuka tarehe 03/10/2020 Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ambaye alikuwa ni Mwenyekiti wetu wa Chama cha Mapinduzi alikuja Zanzibar kuomba kura na kumnadi mgombea wetu kwa wakati ule mgombea kupitia tiketi ya CCM ambaye sasa ndio Rais wetu Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi katika viwanja vya Mnazi Mmoja. Siku ile katika viwanja vya Mnazi Mmoja Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi akiwa mgombea wetu wa Chama cha Mapinduzi aliahidi akasema pindipo atakapochaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi basi atahakikisha moja ya mambo makubwa anairudishia Zanzibar hadhi yake ya kihistoria kwamba hii ndio ilikuwa *logistic herb, the trading herb* ya *East* aInd *Central Africa* hiyo ndio ilikuwa shabaha na malengo yake makubwa kabisa. Ili twende huko lazima tutekeleze miradi.

Lakini Dkt. John Pombe Magufuli aliposimama kuomba kura na yeye akasema haya yote ambayo ameyaomba au ameahidi Dkt. Hussein Ali Mwinyi nitashirikiana naye bega kwa bega. Akasema na yeye naomba nimnukuu kwamba "Zanzibar ndio itakuwa Dubai ya Afrika". Kwa mnasaba huo, pamoja na hotuba yake aliyokuja kuitoa tarehe 11/11/2020 katika kulifungua Baraza lako Tukufu hili la Wawakilishi naomba ninukuu maneno yake Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi ambaye ndio Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alizungumza maneno haya: "Wananchi wetu wamechoshwa na siasa za uhasama, kuhubiri chuki na visasi ambavyo hazibadilishi hali ya maisha yao kuwa bora zaidi, wanataka Matunda ya Mapinduzi na si simulizi za Mapinduzi na Muungano. Wanachotaka ni kustawi na kufaidika na Matunda ya Mapinduzi kwa usawa bila ya upendeleo wala ubaguzi."

Mhe. Naibu Spika, na mimi nilivyowasilisha mwelekeo huu nilinukuu msamiati mmoja wa Kiingereza naomba na leo niunukuu tena: *"If you are not willing to risk the unusual, you will have to settle for the ordinary".* Haya yote nayanukuu kwa sababu gani. Kwa sababu Rais wetu Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi alivyoonesha dira kwamba anataka kuibadilisha

Zanzibar amekubali kubeba msalaba huo. Nawaombeni Waheshimwa Wawakilishi tumuunge mkono na sisi ambao ametupa dhamana hizi za kumsaidia kazi tutamuhakikishia kwamba tutafanya kazi kwa uadilifu kuhakikisha dhamira na ndoto yake inatimia.

Mhe. Naibu Spika, kwa nini tuna miradi mingi, watu wengi wakasema haitofanyika, historia inaonesha tunafanya nusu, nusu inakaa na nusu inabaki. Ofisi yangu ambayo inashughulika na masuala ya Fedha na Mipango tumejipanga kweli kweli. Miradi yote ambayo tumeiandika, tumeiainisha kwenye mpango wetu ambao nimewasilisha, yote itakwenda kutekelezwa. Tumechelewa sana na hatuna sababu ya kuzidi kuchelewa tena. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, Waheshimiwa Wawakilishi watakubaliana na mimi. Kwa miradi yote hii, kuifanya kwa fedha zetu za ndani hatuwezi, na huko duniani ukipitia *literature* mbali mbali, nchi ya China ambayo ndio wajamaa zaidi mwaka 1988 mradi wa kwanza walioingia ubia na sekta binafsi ulikuwa ni Mradi wa Uzalishaji wa Umeme uliokuwa unaitwa *Shenzen Power* ambao serikali na sekta binafsi waliingia pamoja, seuze sisi ni nani. Kwa hiyo, serikali yetu ya Awamu ya Nane imejikita sasa kuhakikisha miradi yote hii ambayo ni ya kimkakati na muhimu kwa uchumi na ustawi wa wananchi wetu inafanyika. Niwaombe Waheshimiwa Wawakilishi na labda niwaeleze, miradi hii tumeigawa katika maeneo makuu matatu. *(Makofi)*

Kuna miradi ya kimkakati ambayo tutahusisha baina ya serikali na sekta binafsi katika utekelezaji wake. Nyote ni mashahidi kuwa mwezi huu ndani ya siku mia moja za Mhe. Rais tumeweza kusaini mikataba mitatu mikubwa ya makubaliano, ikiwemo ule wa ujenzi wa Bandari ya Mangapwani ambayo hii ndio itakuwa bandari kubwa katika Ukanda wa Afrika Mashariki. Tukizungumzia Mangapwani ni bandari ambayo itajengwa yenye *bars* kuanzia 25 hadi 30. Bandari ya kisasa ambayo itajumuisha sehemu ya bandari kavu, bandari ya makontena, bandari ya mafuta na gesi, chelezo kwa ajili ya matengenezo ya meli, lakini pamoja na hayo tunajenga *facility* kubwa kwa ajili ya eneo la uwekezaji wa viwanda vidogo vidogo na vya kati pamoja na maeneo ya uhifadhi *(storage warehouse)*.

Sambamba na hayo, tutakuwa na mji mkubwa wa kisasa katika eneo hili yaani *The Satellite City*. Sio hivyo tu, tumesaini makubaliano ya ujenzi wa Bandari ya Uvuvi ya Mpigaduri nayo itakuwa ni *The State of Art* katika Afrika Mashariki. Bandari itajumuisha uvuvi, viwanda na majokofu kwa ajili ya utunzaji wa samaki, lakini pia tutakuwa na kituo ambacho kitatoa elimu kwa ajili ya sayansi hizi za baharini yaani *Marine Science*, pamoja na uendelezaji na uboreshaji wa Bandari ya Mkoani. Sio hivyo tu, tumeanza safari pia tumeingia makubaliano ya ujenzi au uzalishaji wa umeme kupitia gesi. Safari imeanza kama nilivyoeleza.

Mhe. Naibu Spika, eneo la pili, tutakuwa na miradi ambayo itafanywa na sekta binafsi kwa asilimia mia moja. Hapa serikali haitoshiriki, sekta binafsi kupitia wizara zetu zitahamasishwa kuja kuwekeza Zanzibar. Lakini eneo jengine kuna miradi itafanywa na serikali kwa sababu ya maumbile yake, umuhimu na kwa sababu ya kimikakati ya kiserikali na miradi hii tutaifanya serikali kupitia fedha zetu za ndani na mikopo.

Wenzangu wamezungumza kuwa bado tunakopesheka, deni letu ni himilivu, hatuna haja ya kuogopa na nikuhakikishieni Waheshimiwa Wawakilishi deni letu kwa vile ni himilivu na hatutaki kukawia tutakwenda kukopa ili kuhakikisha miradi yote hii tunaifanya. Naomba nitoe baadhi ya takwimu. Deni letu ukililinganisha na uchumi ni asilimia 22 yaani *the debt to GDP ratio*. Wenzetu walioendelea ambao wao ndio wapo kwenye uchumi wa kwanza naomba ninukuu ili mjue wenzetu wapo katika hali gani. Kwa mujibu wa taarifa za Benki

Kuu na Shirika la Fedha Duniani, Marekani imefika asilimia mia moja na thelathini na moja ya *debt to GDP ratio*. Sisi bado tupo 22, Ufaransa wana asilimia 118, Ujerumani wana asilimia 73.3, Uingereza asilimia 100.8, Canada asilimia 114.6. Kwa hiyo, bado deni letu ni himilivu, tusihofu na hatuna haja ya kuhofu, tutaendelea kukopa lakini pesa hizi zote tutazikopa kwa ajili ya kwenda kutekeleza miradi ya maendeleo ambayo italeta uchochevu wa uchumi wetu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, ili tuendelee tumeingia katika nchi za uchumi wa kati. Lengo letu ni kufika katika nchi zenye uchumi wa ile *the upper level*. Kwa muda huu wa miaka mitano ya awamu hii ni lazima tukue kwa asilimia kumi. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf alizungumzia na mimi nilifurahi sana na mchango wake. Alisema kwa mikakati na mipango hii, tukifanikiwa huenda mapato yetu na ukuaji wa uchumi ukaimarika. Hiyo ndio dira yetu twende huko. Kwa hiyo, miradi hii yote tuliyoiweka inakwenda kujenga msingi na uchochezi mkubwa wa uchumi wetu ambao kwanza tumejifunza kutokana na somo la *Corona*. Uchumi wetu kwa kiasi ulikuwa *pegged* na uchumi wa utalii, ambavyo uchumi wa utalii ulipoathirika na *Corona* basi sekta zote za kiuchumi zilikuja chini kwa sababu biashara ilikuwa inategemea utalii, kilimo kinategemea utalii, uvuvi unategemea utalii. Kwa hiyo, utalii ulipoathirika kutokana na janga hili la *Corona* basi sekta zote zilidorora, ambapo sasa kwa mikakati, malengo na mipango hii tunakwenda ku-*diversify* kupanua uchumi wetu, ili usiwe tegemezi pekee la uchumi wetu kuwa ni utalii.

Uchumi wetu utategemea sasa biashara za kimataifa, uzalishaji wa viwandani, utategemea pia na ufugaji bora ambao wenzangu walikwisha kueleza hapo awali. Lakini ili kufikia haya hatuwezi kufikia tu kwa kusema. Kuna mipango madhubuti ambayo tumeipanga na tumeiainisha, moja wapo ambayo tumeshaanza kuyafanyia kazi ni kuanza kwa baadhi ya *review*.

Mhe. Naibu Spika, la kwanza ni kuja na mpango mzuri ambao utasaidia ufanyaji mzuri wa biashara Zanzibar. Tunaandaa *blue-print* ambayo itasaidia au kurahisisha ufanyaji wa biashara yaani *the easy of doing business*. Wenzangu pia walichangia na nipende tu kuwafahamisha, tuna suala la *regulatory*, hivi vyombo vya udhibiti. Mkakati uliokuwepo serikalini ni kuvipitia upya na kuangalia namna gani tunavipanga na namna gani tunaviweka vyombo vyetu vya udhibiti kwa ajili ya kusaidia ufanyaji wa biashara ndani ya Zanzibar na Tanzania pia katika Kanda zetu kuu za kiuchumi yaani ile ya *East African Community* na ile ya *SADC*. Hii tutaifanya kwa kupunguza vyombo, tuwe na vyombo vichache ili kusaidia kupunguza gharama kwa biashara, lakini pia vyombo vyetu kwa vile tunavilenga kufanya biashara za kikanda na kimataifa ni lazima tuwe na mfumo thabiti katika kudhibiti lakini pia kwenye *standardization*. Tuanze kutumia viwango ambavyo vinakubalika na taasisi nyengine ndani ya jumuiya zetu.

Mhe. Naibu Spika, Wawakilishi wengi walizungumzia eneo la mapato na mimi niungane na wao. Serikali ni lazima tupate mapato kwa ajili ya uendeshaji na mkakati wetu mkubwa sasa kwenye suala la mapato kwanza kuna mapato ya kodi na mapato yasiyo ya kodi. Tuna changamoto mimi nakubali lakini tumeweka mikakati mizuri ili kuhakikisha tunaongeza ufanisi katika eneo hili la kodi.

Mhe. Naibu Spika, mkakati mmoja wapo ni kuongeza wigo wa kodi, tutaongeza wigo yaani tuta-*broaden the tax base*. Kwa kufanya hivyo, tutakuwa na walipa kodi wengi ambao sasa tutapunguza mzigo kwa wale wachache ambao walikuwa wanalipa. Kwa sababu sasa hivi ukienda kwenye Mamlaka zetu za Kodi, walipa kodi wote ambao tumewasajili ni 14,000.

Katika nchi yenye watu takribani milioni moja na laki tano ukienda kwenye *data base* zetu za walipa kodi kuna watu 14,000. Kwa hiyo, hawa watu 14,000 ni lazima watakuwa wamebeba mzigo mkubwa sana. Ili tuondokane na huko ni lazima sasa tuongeze wigo wa kodi ambao tutawatua hawa 14,000 ambao ni kwa muda mrefu walikuwa wanaubeba peke yao. Kwa hiyo, hili litasaidia kwanza kupunguza viwango vya tozo na kodi mbali mbali kwa sababu watu wote ambao watastahiki kuingia kwenye *tax net* tutawaingiza na kwa kufanya hivyo wale wachache nao watafungishiwa vile viwango ambavyo tunatoza kodi.

Sambamba na hivyo, tunahitaji mifumo mizuri na imara ya utozaji kodi ambao tutahakikisha tunakuja na mifumo ya kielektroniki. Hii iliyokuwepo tunaiboresha zaidi ambapo kwa upande wa *ZRB* na *TRA* zote kwa pamoja mifumo yao tunakwenda kuifanya ionane, yaani tuna- *integrate* mifumo hii ya kodi.

Mhe. Naibu Spika, sambamba na hilo, dunia ya leo ni ya kidigitali, mtakubaliana na mimi Waheshimiwa Wawakilishi ule mtindo wa kutoa risiti kwa vibuku umepitwa na wakati. Niliulizwa swali hapa siku moja kuhusu mkakati wangu na nikaeleza, itakapofika tarehe 1 Aprili, natumia nafasi hii pia kuwaambia wafanyabiashara wote, tutakwenda sasa kwenye mfumo wa utoaji wa risiti kwa njia ya kielektroniki, ambapo sasa wafanyabiashara wote tutaona mapato na mauzo yao hapo hapo. Ukitoa risiti tu kule kwenye *server* zetu zinaonesha, kule kwenye *server* zetu zinahesabu kodi yetu ni kiasi gani. Lakini pia tutakuja na mfumo mzuri wa uboreshaji wa forodha. Nchi yetu nilisema lengo la Mhe. Rais ni kuifanya Zanzibar kuwa ndio *The Eastern African Trade Hub*, yaani hapa ndio Kituo cha Ufanyaji wa Biashara.

Tumeshaanza mikakati kwenye forodha ili kuhakikisha ufanisi na utendaji wa watu wetu wa forodha na bandarini. Lakini vile vile, eneo kubwa sasa ni kuwa na viwango ambavyo vitasaidia kutufanya sisi kweli tuwe *trader*s. Viwango vyetu vya utoaji au utozaji wa kodi yaani ile *evaluation base* ya *customs* tutaitengeneza kiasi cha kwamba watu wote watavutika kuja kufanya biashara Zanzibar. Niwaombe tu wafanyabiashara kama Mhe. Rais alivyosema kwamba yeye si muumini wa kodi kubwa na niwahakikishie na sisi tuungane nae na itakapofika bajeti yetu hapa tutakapokuja kuisoma katika Baraza linalokuja mtajionea kwamba eneo hili tumelifanyia kazi kwa kiwango cha juu kabisa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, eneo jengine kwenye kodi ambalo leo hii tuna changamoto kubwa sana ya kiuendeshaji, tuna mamlaka mbili ambazo zinasimamia au zinajishughulisha na suala la kodi. Tuna Mamlaka ya Mapato Tanzania na tuna Bodi ya Mapato ya Zanzibar. Vyombo hivi kuwa viwili kwanza vinapelekea usumbufu na gharama kwa wafanyabiashara wetu, lakini pia baadhi ya wakati vinapunguza hata ufanisi wa ukusanyaji wa kodi zenyewe.

Mkakakati wetu kwanza, kwa vile jambo hili lipo kikatiba. Lakini katika kipindi cha muda mfupi na muda wa kati ni kuhakikisha vyombo vyetu hivi vinafanya kazi kwa pamoja. Tutakuwa tuna *One Stop Centre* ya kodi, wafanyabiashara wetu wakienda kukaguliwa watakaguliwa kwa pamoja na mamlaka zote mbili, sio leo aende *ZRB*, kesho aende *TRA*, akija kukaguliwa na *TRA* maana yake hapo zote mbili zitakuwepo, zitampunguzia usumbufu, gharama na naamini zitasaidia sana kufanikisha biashara zao.

Mhe. Naibu Spika, eneo jengine kubwa katika suala la kodi ni kupunguza utitiri wa kodi na tozo. Baadhi ya hapo tumeshaanza kuzifanyia kazi, nyengine zinasubiri sheria, tutazileta katika Baraza linalokuja tutakapoleta *Finance Bill.* Kwa zile ambazo hazikutaka sheria tumeshaanza kuzipunguza na nyengine kuziondosha kabisa. Hii yote ni kuendana na kauli ya Mhe. Rais kwamba hapa ndio kitovu cha biashara katika ukanda huu.

Lakini pia tuna mapato yasiyo na kodi ambayo mapato hayo yanatokana na tozo au maduhuli mbali mbali yanayotozwa na taasisi za serikali na mawizara yetu. Lakini pia tuna mapato ambayo yanatokana na magawio ya mashirika. Wengi Waheshimiwa Wawakilishi nakubaliana na nyinyi kwamba moja ya changamoto kubwa ambayo ipo katika eneo hili lakini pia nini mkakati wetu. Itakapofika tarehe mosi Julai tumejiwekea lengo, ili tuwe na mfumo madhubuti wa kielektroniki pia ambao utasimamia ukusanyaji wote wa mapato na maduhuli ya serikali. *(Makofi)*

Mimi naamini ukifanya kazi sasa, mianya na mivujo ya mapato yetu itakuwa ndio muarubaini wake. Mapato yote ambayo yatakusanywa moja kwa moja yataripotiwa benki na pia ndani ya hazina yetu. Leo hii mtakubaliana na mimi, mtu akiwa na kitabu cha risiti akitoa risiti hadi ukakague, risiti hii pesa zake zilipelekwa benki au hazikupelekwa inachukua muda mrefu na huenda watendaji ambao sio waaminifu wamechukua mwanya huo kwa kukwepesha au kupoteza mapato mengi ambayo serikali ilikuwa ipate. Kwa hiyo, kwa kuja na mfumo huu wa kielektroniki yaani *the electronic payment detail* itakuwa napo ni muarubaini wao.

Lakini Mhe. Naibu Spika, mashirika yetu, wengi walizungumza kwenye upande wa mashirika. Mashirika yetu mengi hayafanyi vizuri, tuliyokuwanayo ni manne tu katika mengi ambayo yanatoa gawio serikalini.

Mhe. Naibu Spika, Serikali wa Awamu ya Nane imeweka mkakati thabiti ili kuhakikisha mashirika yetu kwanza yanajiendesha kibiashara na nawaombeni sana Waheshimiwa Wawakilishi mtusaidie katika hili. Nyinyi ndio muwe viongozi wa mfano, lakini pia muwe ma-*champion* wa kuwaeleza wananchi wetu malengo ya mashirika yetu kwamba sio ya msaada bali ni ya biashara. Sisi wawakilishi wengine tumekuwa ni sehemu ya kurudisha nyuma utendaji wa mashirika yetu. Kwa hiyo, niwaombeni sana, mashirika yetu haya lengo tulilojiwekea yaende yakafanye kazi kwa ufanisi, kibiashara na yaende yakatoe huduma ambazo zimepangwa kwa mujibu wa uanzishaji wao.

Mhe. Naibu Spika, sambamba na hayo, wizara yangu imepanga kuleta Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Chombo Maalum ambacho kitasimamia Mashirika yetu. Tutaleta Mswada wa Sheria ya Uanzishaji wa Ofisi ya Msajili wa Hazina ambayo ofisi hii au Msajili wa Hazina huyu atakuwa na mawanda mapana ya kusimamia mashirika yetu. Tunaamini kuanzishwa kwa ofisi hii sasa mashirika yetu yatakwenda kusimamiwa vizuri na ipasavyo kuanzia kwenye usimamizi wa miradi na uwekezaji wake, usimamizi wa magawio, mambo kama *return on investment*, namna mitaji iliyowekezwa *versus* mapato yanayopatikana, masuala ya gharama za matumizi yao katika kazi za kawaida na kazi za maendeleo. Kwa hiyo, huko ndio sehemu ambako tumejielekeza kwenye upande wa mapato.

Mhe. Naibu Spika, kwenye upande wa matumizi Waheshimiwa Mawaziri walichangia humu, kuwa na mapato ni sehemu moja, lakini kuwa na watumiaji wa hayo mapato ni sehemu nyengine. Serikali kupitia mpango huu tumejielekeza sasa kwenda kuwa na usimamizi imara wa mapato yetu. Katika *framework* ya miaka mitatu jambo kubwa kabisa ambalo tunataka twende tukalifanye kwanza, *budgetarycControl*, bajeti ikishapitishwa basi matumizi yaendane na bajeti. Hilo ndio eneo la kwanza na kwa kufanya hivyo ndio mipango yetu tutakapoifanikisha, lazima tuwe na *budget discipline* ndani ya serikali. Tukipanga tufanye hichi tukaweka pesa katika kufanya hicho basi ziende zikatumike katika kutekeleza hilo. Kufanya hivi tuna mkakati wa kuja sasa na mfumo wa akaunti moja ya hazina *(the treasury single account).* Waheshimiwa Wawakilishi hii ni dhana mpya naamini tukipata wasaa huko mbele ya safari tutakuja kufahamishana namna gani akaunti moja ya hazina inafanya kazi.

Mhe. Naibu Spika, eneo jengine tumejielekeza katika kuimarisha mifumo yetu ya kielektroniki ndani ya taasisi zetu ambapo itahusisha mfumo mkuu wa matumizi ya serikali pia mifumo ya manunuzi. Tutakuwa na mifumo ya manunuzi sasa. Watu wengi wamezungumzia suala la *procurement,* tunatoka sasa kwenye *procurement* ya kawaida tunakwenda kwenye hii *procurement* ambayo watu sasa watashindana kupitia mifumo ya uwazi ambayo naamini itafanya sasa mashindano yawe ya uwazi, yenye tija na yenye ubora. Kwa kufanya hivyo naamini matumizi ya serikali yataimarika. Hii itakwenda sambamba kwamba matumizi haya ya tenda yatatokana na *LPO* za *procurement,* yatakwenda sambamba na bajeti zile ambazo Waheshimiwa Wawakilishi tutazipitisha.

Mhe. Naibu Spika, eneo jengine kubwa ambalo limezungumzwa na Waheshimiwa Wawakilishi ni suala la usimamizi. Watu wengi walisema tunaweza tukafanya yote tukatenga pesa lakini sasa je, nani anasimamia yale tuliyoyapanga, yale tuliyoyatumia yanafanikiwa. Moja ya jambo kubwa ambalo tumeweka mkakati mkubwa na mkazo kuhakikisha vyombo vyetu vyote vya usimamizi ikiwemo Baraza lako la Wawakilishi Mhe. Naibu Spika, vyote hivi tunavitengea fedha na nyenzo za kutosha katika kufanya kazi zao za *over site.* Lakini kwa upande wa zile taasisi ambazo zipo ndani ya serikali kwanza tumeboresha Idara yetu ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani *(CAG),* kazi yake kubwa tuliyompa ni ukaguzi wa hesabu, sasa tumemtaka mkaguzi wetu wa ndani yeye aende akafanye ukaguzi wa ubora asiende kupitia vitabu tu. Tuta-*equip* idara hii na *engineers, quantity surveyors, technicians* na wataalam wa fani mbali mbali katika miradi mbali mbali ambayo itakuwa inatekelezwa. Kwa hiyo, wakaguzi wetu wa ndani sasa badala ya kuwa ni wahasibu tu kama ilivyozoeleka, sasa tutakuwa na wakaguzi wataalam wa majengo, wahandisi na kadhalika. *(Makofi)*

Lakini suala jengine kwenye Tume ya Mipango pia tuna kitengo maalum ambacho kinashughulika na usimamizi na ufuatiliaji wa miradi. Kitengo hiki nacho tutakiboresha kwa sababu ni kitengo muhimu huwezi ukazungumzia miradi hii yote ya mabilioni ya pesa bila ya kuwa na usimamizi. Tulichojipanga kuhakikisha vyombo vyetu hivi vinafanya kazi kwa ufanisi ambapo vitakuwa na tija kuhakikisha fedha yote ambayo imeelekezwa huko imetumika vile ambavyo tulikusudia.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kueleza maeneo hayo machache, naamini maeneo mengine yote mawaziri wa kisekta waliyachangia na mimi naona sina haja ya kuyarudia. Sasa Mhe. Naibu Spika, niombe Baraza lako la Wawakilishi liridhie Mwelekeo huu wa Hali ya Uchumi, Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Serikali kwa miaka hii, basi ni pamoja na maoni yao sisi watu wa Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango twende tukafanyie kazi na kuleta sasa mpango huu rasmi katika Baraza linalokuja la Wawakilishi. Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**Mhe. Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:** Mhe. Naibu Spika, naafiki.

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, Mhe. Waziri ametoa hoja wale wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, nichukue fursa hii adhimu kwanza kabisa kuwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe na vile vile niungane nao kwa kutoa salamu za

pole kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, pamoja na familia ya Marehemu Maalim Seif Sharif Hamad, pamoja na wanachama wa chama cha *ACT* Wazalendo na Wazanzibari na Watanzania wote kwa msiba ambao umetupata. Mwenyezi Mungu amlaze mahala pema peponi. Amin.

Waheshimiwa Wajumbe, jengine ni kwamba niwashukuru na niwapongeze sana kwa michango yenu mbali mbali mliyoitoa. Michango hii ambayo mmeitoa iko katika uhalisia kabisa na mimi nashukuru sana kwamba tuko hapa kwa ajili ya kuisaidia serikali lakini vile vile kuisaidia nchi yetu. Nashukuru michango ni mizuri sana nilikuwa nasikiliza kwa makini na Waheshimiwa Wajumbe kwa kweli mnachangia vizuri sana na inavyoonesha kwamba mnafanya tafiti kabla ya kusimama kuchangia.

Waheshimiwa Wajumbe, lakini nimpongeze sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kasi yake ya maendeleo ambayo tunaiona sisi wenyewe pamoja na Wazanzibari wote, lakini vile vile namna gani serikali yake inavyofanya kazi.

Vile vile nimpongeze Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha na Mipango ambaye kwanza ametutosheleza kwa yale yote ambayo tulikuwa tuna hofu nayo, lakini vile vile ametupa darasa zuri wapi tunaelekea na mipango gani itafanyika. Mhe. Waziri tunakushukuru sana na tunakuombea kila la kheri Mwenyezi Mungu akusaidie. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, baada ya kusema hayo machache, sasa naomba nitangaze matangazo mawili. Tangazo la kwanza ni kuhusiana na semina ambazo leo zitakuwepo. Napenda kuwakumbusha kuhusu semina za mafunzo tulizozipanga katika mkutano huu wa Baraza. Semina zetu zitaanza mara baada ya kuakhirisha kikao chetu cha Baraza cha asubuhi hii. Semina hizo zinalenga kutoa mafunzo muhimu kwa Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kwa madhumuni ya kuwaelimisha kuhusu jumuiya mbali mbali za kibunge ndani ya Baraza letu kabla ya kufanya chaguzi za jumuiya hizo siku ya Alkhamis tarehe 25/02/2021. Semina hizo zitafanyika leo Jumatatu. Kwa siku ya leo tutakuwa na semina zifuatazo:-

Moja, ni semina kuhusu Masuala ya Kupambana na Rushwa itakayowasilishwa na watendaji kutoka *ZAECA*. Pili, ni semina kuhusu Mtandao wa Wabunge wa Kupambana na Rushwa Afrika *(APNAC)* itakayowasilishwa na mtendaji kutoka Baraza la Wawakilishi. Semina ya tatu, ni kuhusu Mabadiliko ya Tabia Nchi itakayowasilishwa na mtendaji kutoka Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar. Semina ya nne, ni kuhusu Chama cha Mabunge ya Nchi za Jumuiya ya Madola Kanda ya Zanzibar *(Commonwealth Parliamentary Association - CPA)* ya Zanzibar na Chama cha Wabunge Wanawake wa Nchi za Jumiya ya Madola Kanda ya Zanzibar *(CWP)* itakayowasilishwa na mtendaji kutoka Baraza la Wawakilishi. Waheshimiwa Wajumbe, nadhani mmenifahamu vizuri.

Tangazo la pili, Waheshimiwa Wajumbe tunakumbushwa kwamba kulikuwa na mchango tulioahidi kuutoa kwa watoto mayatima ambao mchango huo bado haujawasilishwa. Tunafahamu kwamba kuna wengine tayari wameshawasilisha. Kwa hiyo, wajumbe wote mnaombwa muwasilishe mchango huo ili uweze kufikishwa katika eneo ambalo tumelikusudia.

Baada ya kusema hayo, sasa nimuombe Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais lakini tumemaliza shughuli leo kwa hiyo Katibu. Waheshimiwa Wajumbe kwa taarifa hiyo, sasa naakhirisha kikao hichi hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 6:53 mchana Baraza liliakhirishwa mpaka tarehe 23/02/2021 saa 3:00 asubuhi)*